epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US

# Nipashe

Ijumaa Aprili 26, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581658

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital




**KLOPP AKATA TAMAA EPL**

UKURASA 22

**RC** Dendego kikaangoni kwa kauli yenye utata



UKURASA 3

**Wazazi** wataka tamko la pamoja ufungaji wa shule



UKURASA 4

**Serikali** na NMB kuboresha mifumo ukusanyaji mapato

UKURASA 17



Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, Salum Hamduni

# Utata waibuliwa wizara kuingilia zabuni ya bil.10/-

- **Tenda** yatenguliwa, akarejeshewa mzabuni yuleyule kwa bei kubwa; TAKUKURU yachunguza vigogo wizarani, taasisi nyeti... *Endelea ukurasa 2*

## Mbaroni madai utoroshaji wa chakula msaada mafuriko UK. 3




UKURASA 2

Daladala zikiwa zimetelekezwa baada ya kushindwa kupita kwenye mafuriko katika barabara ya Morogoro, eneo la Jangwani, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Maafa mvua kila kona





OFA KATIKA TOLEO MAALUM!!

Katika kuadhimisha Siku ya Muungano mwaka huu, tarehe 26 April 2024 Kampuni ya The Guardian Ltd (TGL) inayochapisha magazeti ya Nipashe na The Guardian Itatoa toleo maalum la Muungano, hivyo inawakaribisha kutoa salamu za kumbukizi, matangazo, picha na makala za mafanikio katika kusherekea miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar kwa PUNGUZO MAALUM

Wahi mapema kwa sikukuu hii upate PUNGUZO, Artwork ya bure na nafasi katika majukwaa yetu ya kidigitali.

*vigezo na masharti kuzingatiwa*

The Guardian Nipashe

KWA MAWASILIANO TUPIGIE | +255 677 020 701

Barua pepe: advertise@guardian.co.tz Au Tutembelee The Guardian Limited, Mikocheni Light Industrial Area, Mkabala na ITV / Radio One, Dar es Salaam
Tovuti: www.ippmedia.com / epaper.ippmedia.com



Rais Samia Suluhu Hassan, akiongoza Kikao cha Baraza la Mawaziri katika Ikulu Chamwino, mkoani Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

# Utata waibuliwa wizara kuingilia zabuni bil 10/-

**Na Mwandishi Wetu**

UTATA umeibuliwa kuhusu hatua ya Wizara ya Maliasili na Utalii kuingilia zabuni ya Sh. bilioni 9.8 katika Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA) na kusababisha hasara kwa serikali.

Meneja Programu na Utafiti wa Taasisi ya WAJIBU, Moses Kimaro aliibua utata huo alipowasilisha uchambuzi uliofanywa na taasisi kuhusu Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa Mwaka 2022/23.

Kimaro alisema kuwa katika uchambuzi wao, wamelipa kipaumbele suala hilo kwa kuwa ni miongoni mwa hoja kubwa zinazogusa maslahi ya umma.

Alifafanua kuwa CAG amebaini NCAA ilitoa zabuni Na. EA/055/2020-2021/HQ/W/01 kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya makao makuu ya mamlaka hiyo. Zabuni hiyo ilipata mshindi Machi 9, 2022 baada ya kupitia mchakato wa kisheria kutekeleza mradi wenye gharama ya Sh. bilioni 9.8.

Hata hivyo, Kimaro alisema kuwa CAG amebaini kuwa Aprili 21, 2022, yaani siku 12 baada ya mshindi kutangazwa, zabuni hiyo ilisitishwa kutokana na maelekezo ya Wizara ya Maliasili na Utalii.

"Inaripotiwa na CAG kuwa NCAA ilielekezwa na wizara kusitisha zabuni hiyo na kuanza upya mchakato wa kuitangaza," alisema.

Kimaro aliendelea kurejea ripoti ya CAG, akisema kuwa zabuni ilitangazwa upya Mei 6, 2022, na mzabuni yuleyule aliyeshinda awali alitwaa tena zabuni hiyo, safari hii thamani yake ikipanda kwa Sh. milioni 686.6 ndani ya miezi miwili kutoka Sh. bilioni 9.8 hadi Sh. bilioni 10.48. Gharama za mchakato mpya wa zabuni ni Sh. milioni 16.08.

**TAKUKURU**

Akichangia kuhusu hoja hiyo, Joseph Mwaiswelo, Mkurugenzi wa Elimu kwa Umma wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), alisema wanachunguza baadhi ya watendaji wa NCAA na taasisi zingine za serikali kutokana na kutajwa na CAG kuwa na viashiria vya rushwa kiutendaji.

Mbali na NCAA, Mkurugenzi Mwaiswelo aliwataja watendaji wengine ni pamoja na wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA).

"Kifungu cha 27 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma inamtaka CAG wakati wa ukaguzi akibaini jambo lenye viashiria vya rushwa, atoe taarifa kwa TAKUKURU.

"Kwahiyo, sisi (TAKUKURU) hatusubiri hadi ripoti ya CAG itoke ndipo tuanze kufanya ufuatiliaji, Hata hao NCAA tunawachunguza. Na si wao tu, tunachunguza pia TANAPA na TANESCO," alisema.

Mkurugenzi huyo pia alitoa ufafanuzi kwanini ripoti ya mwaka ya utendaji wa TAKUKURU huwa haiwekwi wazi kwa umma, akisema sheria haijatamka iwekwe wazi kwa umma baada ya kuwa wameiwasilisha kwa Rais.

"Lakini pia kwenye ile taarifa huwa tunataja hadi majina ya watu tunaowachunguza. Hii ndiyo inaweza kuwa sababu ya taarifa hii kutokuwa wazi kwa umma. Mle ndani pia mna taarifa ambazo ni za siri," alisema.

Alibainisha kuwa katika kufanyia kazi ripoti iliyopita ya CAG, TAKUKURU ilifungua majalada ya uchunguzi 375. Kati yake, 156 yalikosa ushahidi wa kufikishwa mahakamani, 73 yalichukuliwa hatua, 28 yako kwa Mkurugenzi wa Mashtaka na 41 yalitolewa hukumu mahakamani, wakishinda 40 na kushindwa katika shauri moja.

**TANESCO**

Katika wasilisho lake, Kimaro alisema TANESCO ina hoja nyingi, ikiwa ni pamoja na kutoshughulikia kwa miaka minne malipo ya Sh. bilioni 262.34 zinazopaswa kutolewa na mkandarasi wa Mradi wa Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere (JNHPP).

Vilevile, kutimiza mahitaji ya kisheria ya kulipa wazalishaji binafsi wa umeme (PAP) Sh. bilioni 11.43, uamuzi unaotia shaka wa kubadili mita za umeme 108,088 kabla ya kuishi kwa muda wake wa matumizi.

Katika uchambuzi wake, Taasisi ya WAJIBU pia imegusia mwenendo usioridhisha wa utoaji huduma za afya ya akili nchini, hasa ngazi ya jamii.

**HALI YA RUSHWA**

Kimaro alisema upimaji wa viashiria vya rushwa (CPI) kwa mwaka 2023, uonesha Tanzania inafanya vizuri, ikishika nafasi 87 kati ya 180 zilizofanyiwa tathmini duniani.

Hata hivyo, meneja huyo alisema uchambuzi wa Taasisi ya WAJIBU umebaini kuwa kwa mwaka 2022/23, Sh. trilioni 2.778 ziko hatarini kupotea katika mazingira yenye viashiria vya rushwa na udanganyifu sawa na asilimia saba ya bajeti yote ya serikali kwa mwaka wa fedha 2022/23, ambayo ilikuwa Sh. trilioni 41.48.

"Tumebaini kuwa viashiria vya rushwa vimeoungua kwa asilimia 10 mwaka 2022/23 kulinganisha na mwaka 2021/22, ambao vilikuwa vya Sh. trilioni 3,084," alisema Kimaro.

Alifafanua kuwa kati ya Sh. trilioni 2.778 zilizo hatarini kupotea katika mazingira yenye viashiria vya rushwa, ubadhirifu na udanganyifu kwa mwaka 2022/23, mashirika ya umma yana Sh. bilioni 1,234.67, Serikali Kuu Sh. bilioni 676.66, Serikali za Mitaa Sh. bilioni 641.29 na miradi ya maendeleo Sh. bilioni 225.39.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya WAJIBU, Ludovick Utouh (CAG mstaafu), Msajili Msaidizi - Fedha na Utawala katika Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB), Paul Bilabaye na Ofisa Ununuzi Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Ununuzi wa Umma (PPRA),Alice Mcharo walisema nchi inaendelea kushuhudia ubadhirifu wa fedha za umma kutokana na viongozi kukosa uzalendo.

# Mvua yaua saba na kujeruhi Kilimanjaro

**Na Waandishi Wetu**

WATU saba, wakiwamo watoto wa familia moja, wamefariki dunia katika wilaya ya Moshi, Kilimanjaro na wengine kadhaa wakijeruhiwa, huku kaya na miundombinu ikiathiriwa na mvua iliyonyesha usiku wa kuamkia jana.

Mvua hiyo pia imesababisha athari katika wilaya ya Arumeru mkoani Arusha kwa baadhi ya wananchi kupoteza makazi, huku barabara ya Arusha -Moshi ikifungwa kwa saa kadhaa baada ya kukata mawasiliano eneo la King'ori.

Aidha, zaidi ya magari 800, yakiwamo mabasi ya yanayotoa huduma za usafirishaji abiria, kati ya mikoa ya Kilimanjaro na Arusha, kwenda Kanda ya Ziwa, Dar es Salaam na Kanda ya Kati, yalilazimika kukatisha safari kwa zaidi ya saa nne kusubiri kurejea kwa mawasiliano ya barabara.

Kaya zilizoko Msaranga na kata ya Mji Mpya mjini Moshi, zimepoteza mali, vyombo vyote vya ndani, chakula, wengine kulala nje baada ya makazi yao kubomolewa na maji yaliyotokana na kufurika na kumong'onyoka kwa kingo za Mto Rau.

Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, alisema jana miili iliyoopolewa kutokana na maafa ya mvua hadi jioni ilikuwa imefikia saba.

Alisema kati yake ni watoto watatu wa familia moja waliopoteza maisha kwa kuangukiwa na ukuta katika Kata ya Kimochi, Moshi Vijijini, na miili mingine ikiopolewa kutoka katika Mto Rau baada ya kufurika.

Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Marko Ng'umbi, akizungumzia mafuriko yaliyosababisha kukatika kwa mawasiliano ya barabara katika eneo hilo, alisema licha ya mvua hiyo kuharibu miundombinu ya barabara na kukatisha mawasiliano, hakuna madhara yaliyojitokeza kwa binadamu, wala makazi yao. "Ni kweli unajua mvua kubwa ilinyesha usiku katika Mkoa wa Arusha na katika eneo letu la King'ori, maji yote ya mafuriko yalikimbilia barabarani.

"Sasa kwa kuhofia usalama kwa watumiaji wa barabara kuu ya Arusha/ Moshi, kwa maana ya watumiaji wa mikoa ya Kaskazini na kuelekea Ukanda wa Mashariki kwa maana ya Dar es Salaam, Tanga na Morogoro.

"Hatua ya kwanza, ambayo tuliifanya kuepusha ajali ambazo zingeweza kusababisha vifo, ilikuwa ni kusimamisha magari yote yanayotoka Arusha kuelekea Kilimanjaro, na maeneo mengine ya nchi yetu, lakini pia magari yanayotokea Kilimanjaro kuja Arusha.

Kikosi cha Usalama Barabarani kikiongozwa na RTO (Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa), waliweka kambi King'ori na kuyazuia, lakini baadaye ili presha ya maji ilivyopungua tulianza kuruhusu malori ya mizigo na baadaye tukaanza kuruhusu mabasi na magari madogo kawaida," alisema

Mbunge wa Moshi Mjini (CCM), Priscus Tarimo, alisema: "Nilipata simu kuanzia saa 9:00 usiku wananchi wangu wakinieleza kwamba, hali si shwari katika Kata ya Msaranga, ambako mwaka 2020 pia, tulipata matatizo kama haya, kutokana na kingo za Mto Rau kumong'nyoka na kusababisha maji kuingia kwenye makazi ya watu.

"Kwa upande wa Kata ya Mji Mpya, hatujapata madhara ya kifo, lakini taarifa ambayo mpaka sasa haijawa rasmi ni kwamba kuna kifo upande wa Msaranga, na watu watatu bado hawajulikani mahali walipo," alisema. Kwa mujibu wa Mbunge huyo, uharibifu mkubwa umetokea kwenye miundombinu, hasa kwenye nyumba za watu na mazingira kwa ujumla.

"Wito wangu kwanza kwa wale ambao hatujapata madhara haya, tushiriki kwa karibu kabisa kuwasaidia wenzetu ambao wamepoteza vitu, mali na makazi yao kubomoka, ili wapate msaada ambao utawafaa kwa sasa.

"Watu wanaoishi maeneo hatarishi kwa kipindi cha mvua hizi ambazo ni nyingi, wawe makini kuangalia mikondo ya maji na kuchukua tahadhari zote," alisema. Wilayani Same, Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), imefanikiwa kurejesha mawasiliano ya barabara ya Mwembe/ Myamba /Ndugu, yenye urefu kilomita 90.19 kwa kiwango cha changarawe baada ya kukata mawasiliano yake. Ukarabati huo umetumia zaidi ya Sh. bilioni 1.6.

***Imeandikwa na Godfrey Mushi (ARUSHA), Mary Mosha (SAME) na Rahma Suleiman (Zanzibar).**

## HABARI KITAIFA

# Mbaroni madai utoroshaji chakula msaada mafuriko

**Na Julieth Mkireri,** RUFIJI

SERIKALI wilayani Rufiji inashikilia watu 11 wakiwamo watendaji wa serikali kwa tuhuma za kuchepusha chakula cha msaada kinachotolewa kwa ajili ya waathirika wa mafuriko wilayani humo.

Watuhumiwa hao walikamatwa baada ya kukutwa na chakula cha msaada walichoficha wakati wa upakuaji na ugawaji vyakula kwa waathirika katika wilaya hiyo.

Mkuu wa Wilaya ya Rufiji, Meja Edward Gowele amethibitisha kukamatwa watuhumiwa hao, akisema kuwa baadhi yao wameanza kurejesha chakula wanachodaiwa kuiba.

Meja Gowele alisema miongoni mwa waliokamatwa ni Ofisa Mtendaji wa Kata na wa kijiji ambao walikuwa wanasimamia shughuli za upakuaji na ugawaji chakula pamoja na vijana tisa ambao walikuwa wanasaidia shughuli hiyo.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Wilaya, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) inaendelea na mahojiano zaidi na watuhumiwa hao.

Meja Gowele alisema kati ya kata 13 za wilaya hiyo, 12 zimeathiriwa na mafuriko na baadhi ya wananchi wako kwenye kambi baada ya nyumba zao kuzingirwa na maji huku mazao yakiharibiwa.

Juzi Nipashe iliripoti kilio cha waathirika wa mafuriko kuhusu kuchepushwa misaada mbalimbali inayotolewa kwao na wadau mbalimbali, huku wakilalamikia kupewa chakula kidogo kisichotosheleza mahitaji ya kibinadamu huku waliojishikiza kwa ndugu, jamaa na marafiki wakilalamikiwa kutopewa mgawo.

Wakati huo, Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge amepokea hundi ya Sh. milioni 20 kutoka kwa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS).

Kunenge jana alishukuru taasisi hiyo kwa kuungana na wadau wengine kutoa msaada kwa waathirika wa mafuriko wa wilaya za Kibiti na Rufiji, mkoani mwake.

# RC kikaangoni kwa kauli yenye utata

**Na Elizabeth Zaya**

JUKWAA la Elimu kwa Watoto wa Kike, limemjia juu Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, kutokana na kauli aliyoitoa hivi karibuni kwamba msichana atakayepata ujauzito akamatwe na awe mshitakiwa wa kwanza.

Kwa mujibu wa taarifa ya jukwaa hilo, Dendego alitoa kauli hiyo Aprili 21, mwaka huu, akiwa katika ziara ya kikazi katika Halmashauri ya Itigi, alipokuwa akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Kitaraka.

"Sisi kama mashirika yanayounda Jukwaa la Elimu kwa Mtoto wa Kike, tumesikitishwa na kauli hii ya mkuu wa mkoa wa Singida aliyosema: 'nikikuta msichana umepata mimba wewe utakuwa mshtakiwa namba moja na wewe ndiye utakayeenda jela bila huruma na tumbo lako.

"Hakuishia hapo bali alisema 'utajifungulia huko huko kwa sababu mna tabia ukipata mimba tunaenda kukimbizana na mtoto wa kiume si sawa wote mlishirikiana kwa hiyo yeye atakuwa mstakiwa namba mbili na msichana atakuwa mshtakiwa namba moja," ilisema taarifa hiyo.

Kwa mujibu wa jukwaa hilo, kiongozi huyo aliagiza wanafunzi wa kike waliopata mimba wakiwa shuleni kukamatwa na kuchukuliwa hatua za kisheria pamoja na wazazi wao.

"Kauli ya Dendego, inasahau chanzo cha mimba za utotoni katika jamii yetu na kuwahukumu wasichana kama ndio chanzo na suluhu pekee ya kumaliza tatizo la mimba za utotoni.

"Kauli hii inarudisha nyuma jitihada zinazochukuliwa na serikali pamoja na wadau mbalimbali wa elimu katika kuhakikisha tunaondoa vikwazo na kila mtoto anapata fursa ya kupata haki ya elimu," lilieleza jukaa hilo.

Taarifa ya jukwaa hilo ilisema Sheria ya Elimu kifungu cha 60 (3) (Sura ya 353 R.E 2019) kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2016, inafafanua mazingira na adhabu atakayopewa mtu pale anapompatia ujauzito mwanafunzi.

"Sheria hiyo inaeleza kwamba mtu yeyote ambaye amempa mimba mwanafunzi shule ya msingi au sekondari amefanya kosa na, atawajibika kwa kifungo cha kwenda jela muda wa miaka thelathini.

"Sheria ya Kanuni ya Adhabu sura ya 16 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2022 katika kifungu chake cha 130 (1) (e) inasema kuwa mwanaume atakuwa amebaka pale atakapofanya tendo la ngono na binti wa umri chini ya miaka 18. Sheria hizi zote zinatoa ulinzi kamili kwa msichana wa miaka chini ya 18 na mwanafunzi yeyote wa kike bila kujali umri, dhidi ya vitendo vya kingono, ili kumfanya afurahie haki yake ya kielimu," lilifafanua.

Pia lilisema kumkamata binti aliyepata ujauzito ni kuendelea kumkandamiza kwa sababu ndiye mhanga wa vitendo vya ubakaji alivyofanyiwa.

Novemba 2021, serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilitoa Waraka wa Elimu Na. 2, unaoruhusu wanafunzi waliokatiza masomo kwa sababu mbalimbali ikiwamo ujauzito kurejea shuleni katika mfumo rasmi.

Kadhalika, mwaka 2022, ilitoa mwongozo unaotaka wanafunzi kurejea shule ndani ya miaka miwili baada ya kuwa nje ya mfumo rasmi na kwa mujibu wa takwimu za BEMIS 2022 na 2023 wasichana 5,197 wamesharejea shuleni kama utekelezaji wa mwongozo huo.

Jukwaa hilo lilisema kauli hiyo ya Dendego ina lengo la kurudisha nyuma juhudi za serikali ya Tanzania, wadau wa maendeleo na watetezi wa haki za wasichana katika ulinzi wao kielimu.

Pia lilisema kauli hiyo inakwenda kinyume na makubaliano ya utekelezaji wa mkataba wa Afrika wa haki na ustawi wa mtoto ambao Tanzania imeridhia na hivyo kuirudisha Tanzania katika ramani ya wavunjifu wa haki za watoto Afrika.

Nipashe The Guardian

Kutoka Menejimenti ya The Guardian Limited



**Wapendwa Wateja wetu**

Tunayo furaha kutangaza hatua kubwa kuelekea upatikanaji wa magazeti yetu kidijitali. Kuanzia tarehe 13 Aprili 2024, magazeti ya wikiendi ya **Nipashe Jumamosi, Nipashe Jumapili na The Guardian on Saturday** yanapatikana kwa njia ya gazeti-mtandao kupitia **epaper.ippmedia.com** au **www.ippmedia.com**

Siku za wiki (Jumatatu hadi Ijumaa) utaendelea kufurahia matoleo yote, kuchapishwa na Mtandaoni

Asante kwa usomaji wako, na kuendelea kuwa nasi katika mabadiliko haya.

Kwa mawasiliano zaidi Tupigie: 0677 020 701
Subscription: 0625 174 714
Barua pepe: customerrelations@guardian.co.tz



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akijibu maswali yaliyoulizwa na baadhi ya Wabunge kwenye kipindi cha maswali kwa Waziri Mkuu, Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Vifo vya mafuriko vyafikia 155

**Na Vitus Audax,** DODOMA

SERIKALI imesema hadi kufikia jana, madhara yanayosababishwa na mvua inayoendelea kunyesha katika maeneo mbalimbali, yameongezeka.

Madhara hayo, kwam ujibu wa serikali ni vifo 155, majeruhi 236, zaidi ya nyumba 10,000 zimeharibiwa sambamba na kaya 51,000 na watu 200,000 wameathirika.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alisema hayo jana bungeni jijini hapa wakati akitoa taarifa kuhusu athari za hali ya hewa nchini wakati wa kipindi cha maswali ya papo kwa papo.

Alitaja maeneo mengine yaliyoathirika kuwa ni pamoja na miundombinu ya shule, zahanati, nyumba za ibada, barabara, madaraja, mifugo na mashamba yenye mazao mbalimbali.

"Baadhi ya maeneo yaliyoathirika nchini ni pamoja na Rufiji na Kibiti (Pwani), Malinyi, Mlimba, Kilosa, Manispaa ya Morogoro, na Ifakara (Morogoro); Ilala, Kinondoni, Ubungo, Kigamboni na Temeke (Dar es Salaam); Same, Hai na Moshi (Kilimanjaro).

"Pia Mbarali, Kyela na Halmashauri ya Jiji la Mbeya (Mbeya); Manispaa ya Kigoma Ujiji na Kakonko (Kigoma), Iringa Vijijini (Iringa), Manispaa ya Tabora (Tabora), Bahi (Dodoma), Lindi Manispaa, Kilwa, Liwale, na Nachingwea (Lindi), Masasi (Mtwara) na Arusha Jiji, Monduli na Karatu (Arusha),"alisema.

Majaliwa alitaja maeneo mengine kuwa ni Muleba, Manispaa ya Bukoba mkoani Kagera, Manispaa ya Shinyanga, Geita Mji, Nyangh'wale na Chato, Mbozi na Momba (Songwe); Nkasi, Sumbawanga na Kalambo (Rukwa) pamoja na Hanang' (Manyara).

**ONGEZEKO LA MVUA**

Waziri Mkuu alisema uchunguzi umebaini sababu za ongezeko la mvua nchini duniani ni kutokana mabadiliko ya hali ya hewa yaliyosababisha ongezeko la joto kwa mwaka 2023.

Alisema tathmini ya Shirika la Hali ya Hewa Duniani inaonyesha kuwa wastani wa ongezeko la joto kwa mwaka 2023 ulifikia nyuzi joto 1.4 kwa kipimo cha Celsius, hivyo kuvunja rekodi ya mwaka yenye joto kubwa zaidi katika historia ya dunia.

Aidha, alisema kwa Tanzania, wastani wa ongezeko la joto kwa mwaka 2023 ulifikia nyuzi joto 1.0 kwa kipimo cha selsiasi, na pia ulivunja rekodi kwa kuwa mwaka wenye joto kubwa zaidi katika historia ya Tanzania.

**HATUA ZA SERIKALI**

Majaliwa alisema katika kukabiliana na athari za mvua kubwa iliyoanza kunyesha Oktoba hadi Desemba, mwaka jana, ikitarajiwa kumalizika Mei, mwaka huu, ikiwa na ongezeko kubwa la mvua la milimita 534.5 ikilinganishwa na milimita 227.2 kwa mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 135, hatua mbalimbali zimekuwa zikichukuliwa lengo likiwa ni ya kuzuia, kukabiliana na kurejesha hali.

Alitaja hatua hizo kuwa ni pamoja na utoaji wa elimu kwa jamii ya kujikinga na kuchukua tahadhari, kukabiliana na maafa na kurejesha miundombinu iliyoharibika na kutoa misaada ya kibinadamu ikiwemo chakula, vifaa vya ujenzi, vifaa vya malazi na vifaa vya , uokoaji, kutoa vyakula, mahema,dawa, marekebisho ya miundombinu ya utoaji huduma imeendelea kutolewa.

"Serikali imejipanga kikamilifu na inaendelea kuchukua hatua stahiki ili kuzuia na kupunguza makali ya majanga sambamba na kurejesha hali katika maeneo mbalimbali yaliyoathirika,"alisema Waziri Mkuu.

Pia alisema serikali iliandaa mpango wa Taifa wa dharura wa kuzuia na kukabiliana na madhara ya Elnino kwa kipindi cha Septemba 2023 mpaka Juni 2024 sambamba na kuandaa mipango ya dharura katika mikoa 14 iliyokuwa katika hatari ya kuathiriwa na mvua hiyo.

**MAAGIZO YA SERIKALI**

Aidha, Majaliwa aliziagiza taasisi za serikali kukabiliana na maafa kwa kushirikiana na wadau, Kamati za Maafa za Wilaya na Mikoa kuendelea kuchukua hatua stahiki ikiwemo kutoa tahadhari kwa wananchi na kusaidia wananchi kwa wakati pindi maafa yanapojitokeza

Vilevile, aliwataka wananchi wafuatilie taarifa za utabiri wa hali ya hewa zinazotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) na kuzingatia maelekezo yanayotolewa na viongozi katika maeneo yao, ikiwemo kuhamia maeneo salama, kulima mazao yanayopendekezwa.

Aidha, alisema wakuu wa mikoa na wilaya, maafisa tarafa, watendaji kata, mitaa na vijiji wasimamie ipasavyo usafi katika maeneo yao na kudhibiti utupaji taka ovyo unaosababisha kuziba kwa mitaro badala ya kusubiri usafi unaofanyika kila Jumamosi ya mwisho wa mwezi

Alisema viongozi wa ngazi zote washirikiane na wananchi kudhibiti uharibifu wa mazingira katika maeneo yao, kwa shule zilizofungwa kutokana na athari za mafuriko, halmashauri na wamiliki wa shule zisizo za serikali waweke utaratibu wa kufidia muda wa vipindi ili kukamilisha kalenda ya muhula kama ilivyopangwa.

"Niwatake wamiliki wa shule pamoja na madereva kuchukua taadhari wakati wa kusafirisha wanafunzi, pia TARURA TANROADs, TAZARA na TRC ufanye tathmini ya barabara na njia za reli zilizoathirika na mafuriko na kuweka mpango wa kukarabati haraka ili kurejesha mawasiliano. Aidha, wabainishe maeneo yanayopitiwa na mikondo ya maji kote na kuweka alama za tahadhari,"alisema.

Aidha, alilitaka jeshi la polisi kupitia Kikosi cha Usalama Barabarani kuendelee kutoa tahadhari kwa madereva na watumiaji wengine wa barabara wakati wa mvua, Kamati za Maafa katika ngazi za Vijiji, Wilaya na Mikoa zisimamie kikamilifu ugawaji wa misaada inayotolewa kwa waathirika wa mafuriko.

## Wazazi wataka tamko pamoja ufungaji shule

**Na Waandishi Wetu**

BAADHI ya wazazi wameitaka serikali itoe tamko la pamoja kuhusu ufungaji wa shule kwa maeneo yaliyoathiriwa na mvua badala ya kila shule kufanya hivyo na kuleta usumbufu kwao kwa kuchelewa kupokea taarifa kwa wakati.

Jumanne, Kamishna wa Elimu Tanzania, Dk. Lyabwene Mtahabwa, akizungumza na Nipashe, alisema kuna uwezekano wa shule kufungwa, huku Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, akipongeza zilizochukua hatua kutokana na mvua inayoendelea.

Richard Stanley, mkazi wa Tabata, aliiambia Nipashe kuwa utaratibu wa kila shule kujichukulia hatua binafsi hauafiki kwa kuwa ni usumbufu, hivyo ni vyema serikali ikatoa tamko la shule zilizoko katika changamoto zifungwe kwa muda wakati huu wa mvua.

"Mara nyingi wazazi tunapokea taarifa ghafla asubuhi wakati ambao mzazi anakuwa ameshamwandaa mtoto na wakati mwingine akiwa njiani kuelekea shule.

"Hii inakuwa bora yule anayechukuliwa na basi la shule ukiona haliji unajua kuna changamoto, lakini kwa mtoto anayetumia usafiri wa umma ni usumbufu kwake na kwa wazazi pia," alisema.

Mkazi wa Ubungo Maji ambaye hakutaka jina lake liandikwe gazetini, alisema kutokuwapo kwa tamko la pamoja kunawasababishia usumbufu wazazi.

"Mtoto wangu anasoma Masaki, hii ni mara ya tatu ninaondoka naye asubuhi sana kumpeleka shule ili mimi niwahi kazini mjini.

"Tukiwa njiani ndiyo unapokea taarifa ya kutoka shule kuwa masomo hayatakuwapo leo kwa sababu ya mvua, sasa unalazimika kumrudisha mtoto nyumbani, huu ni usumbufu kwetu" alisema.

TAMONGSCO

Mwenyekiti wa Taifa wa Shirikisho la Wamiliki wa Shule na Vyuo Binafsi Tanzania (TAMONGSCO), Leonard Mao, alizishauri shule zilizositisha masomo kutokana na mvua kuhakikisha zinatafuta namna ya kufundisha na kumaliza mitaala kama kalenda ya Wizara ya Elimu inavyoelekeza.

"Kama ikitokea shule imeamua kusitisha masomo kupisha hali ya mvua basi kile kipindi cha mwezi wa sita ambapo shule zinafungwa wanaweza kuendelea na masomo ili kufidia muda wanafunzi waliokaa nyumbani ili kumalizia masomo ya muhula huo," alisema.

Aidha, alizishauri shule ambazo zipo katika mikoa ambayo hakuna adha ya mafuriko na zile ambazo maeneo yao hayajafikiwa na athari zozote kuendelea na masomo na kumaliza mhula kama ilivyoelekezwa kwa kuwa, siku zimebaki ni chache.

**Imeandaliwa na Romana Mallya na Jenifa Gilla**

## HABARI KITAIFA



Mkuu wa Wilaya Same, mkoani Kilimanjaro, Kaslida Mgeni (katikati), akikata utepe kuzindua wiki ya chanjo ya saratani ya shingo ya kizazi (HPV), katika Shule ya Msingi Same juzi, ambapo mabinti wenye umri wa miaka 9-14 wanapatiwa chanjo hiyo. Kushoto ni Mganga Mkuu wa wilaya hiyo, Alex Alexander na Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya wilaya hiyo, Muina Mmasa. **PICHA: ASHRACK MIRAJI**

# Msukuma ataka V8 serikali zifungwe gesi

**Na Vitus Audax,** DODOMA

MBUNGE wa Geita Vijijini (CCM), Joseph Kisheku maarufu kama Msukuma, ametaka magari yote ya serikali, yakiwamo makubwa kama Toyota Landcruiser V8, kufungwa mfumo wa gesi ili kubana matumizi.

Msukuma alisema hayo jana bungeni wakati akichangia makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Nishati kwa mwaka 2024/25.

Alisema kwa kufanya hivyo, matumizi hayo makubwa ambayo yamekuwa yakiripotiwa mara kwa mara katika taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) yanaweza kupungua au kuisha kabisa.

"Kitu nilichojifunza hapa ni kuwa gari kama V8 ukitoka Dar es Salaam kuja Dodoma ukitumia mafuta unatumia kama Sh.500,000 lakini ukitumia gesi unatumia Sh.47,000 sawa na Sh.94,000 kwenda na kurudi.

"Sasa kwa kuwa tunahangaika sana na Mr. Kichere (CAG) kuhusu matumizi mabovu ya serikali. Nashauri V8 zote zifungwe mfumo wa gesi kwa sababu muda mwingi mko Dar - Dodoma kwa hiyo tuwawekee mitungi huko nyuma mkisafiri hata mara tatu serikali itakuwa imepunguza matumizi kwa asilimia kubwa," alisema.

Pia alisema hatua hiyo itasaidia kusukuma hoja ya kuongeza vituo vya gesi kwa ajili ya magari nchini kutokana na mawaziri kutumia mfumo huo ili kila maeneo vipatikane na kuongeza matumizi ya nishati hiyo kwenye magari.

**HUDUMA YA GESI**

Msukuma pia alisema hali ya upatikanaji wa huduma ya kujaza gesi katika magari bado iko chini kutokana na idadi ndogo ya vituo vya kutolea huduma hiyo. Alitaja vituo viwili vilivyoKo Dar es Salaam ndivyo pekee vinavyotoa huduma hiyo, hivyo mtu analazimika kusubiri kwa zaidi ya saa tisa kupata huduma.

"Ukitaka kuweka gesi leo katika vituo viwili vya Dar es Salaam, unaenda saa tisa usiku. Sisi tulifika pale saa 8:00 watu waliopanga foleni wakaanza kusema hawa wabunge wamekuja kufanya nini sisi tunataka huduma hatutaki wabunge wanadai wanasubiria kwa saa tisa," alisema.

Alishauri serikali kupunguza masharti katika utoaji wa huduma hiyo na kuwa serikali itafute njia za kuongeza wawekezaji katika utoaji wa huduma hiyo.

Mbunge wa Kigoma Mjini (CCM), Kilumbe Ng'enda, alishauri serikali kuruhusu sekta binafsi kuwekeza katika utoaji wa huduma ya kusambaza na kuongeza gesi katika magari ili ifike maeneo mbalimbali hususani katika majiji.

"Hali hii itawezesha kuongezeka kwa ufanisi katika utoaji wa huduma hii hivyo serikali isijihangaishe saana katika hili bali iwape wawekezaji kama tulivyofanya kwenye suala la mafuta na tunaona hali ilivyo kwa sasa," alisema Ng'enda.

**MAJIBU YA SERIKALI**

Akijibu hoja kuhusu hoja ya huduma za vituo vya kutolea huduma, Naibu Waziri wa Nishati, Judith Kapinga, alisema tayari serikali imeanza kuchukua hatua za muhimu ikiwa ni pamoja na kuanza ujenzi wa kituo mama cha kujaza gesi Dar es Salaam.

Pia alisema wanajenga vituo vingine kwa ajili ya kumaliza foleni na kwamba vituo hivyo vinajengwa katika maeneo ya Kairuki (Mikocheni) na Muhimbili, Upanga .

"Vilevile tunaendelea na mpango wa ujenzi wa vituo 20 ambavyo vitatekelezwa na sekta binafsi lengo likiwa ni kuhakikisha tunakuwa na huduma hiyo katika maeneo mbalimbali," alisema

# Kambi JKCI yafanya upasuaji watoto 24

**Na Romana Mallya**

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Jakaya Kikwete (JKCI), Dk. Peter Kisenge, amesema kambi ya upasuaji ya kikundi cha Muntada Aid kutoka Uingereza kwa kushirikiana na madaktari wazawa, wamewafanyia operesheni watoto 24, huku wengine 40 wakisubiria huduma hiyo.

Akizungumza maendeleo ya kambi hiyo jana, Dk. Kisenge alisema tangu Jumamosi taasisi ilipokea wageni hao ambao pia, wanasaidia kufundisha madaktari wazawa katika kupasua moyo hasa kwa watoto katika tiba ya tundu dogo.

Alisema tangu kambi hiyo ianze kufanya kazi na JKCI, wameshawafanyia watoto zaidi ya 500 na katika kwa sasa wamepanga kuwafanyia operesheni watoto 60 kutoka Tanzania Bara na Visiwani Zanzibar.

"Mpaka sasa watoto 24 wameshapata matibabu na tunategemea mpaka kambi ikimalizika tutakuwa tumewafanyia watoto 40," alisema.

Alisema kambi hiyo ina muungano wa madaktari mbalimbali kutoka nchi za Misri, Uingereza, Uholanzi na Canada.

Alisema madaktari hao wamekuja Tanzania kutokana na miundumbinu iliyowekezwa katika vifaa tiba na rasilimali watu, ambapo hivi karibuni serikali ilitoa karibu Sh. bilioni tano kwa ajili ya kusomesha madaktari nchi nzima kwenye ubingwa bobezi.

"Wanapokuja wanataka kuona mazingira mazuri ya kufanyia upasuaji, watoto 40 watafaidika. Kama mnavyofahamu operesheni moja akifanyia nchini inaweza kugharimu Sh. milioni 15, lakini tukimpelekea nchini India inafika hadi Sh. milioni 30," alisema.

Dk. Kisenge alisema timu hiyo imekuja na vifaa vinavyokaribia Sh. bilioni 1.5 ambavyo taasisi inaviendeleza kusaidia watoto wengine huko baadaye.



# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Muungano udumishwe ipasavyo, una faida kubwa kwa Watanzania

**MANUFAA** yake ni Muungano wa Tanganyika na Zanzibar uliozaa taifa la Tanzania, leo unatimiza miaka 60 tangu kuasisiwa kwake. Maadhimisho hayo ya miongo sita ya Muungano yanabebwa na kaulimbiu isemayo: "Tumeshikamana na Tumeimarika, kwa Maendeleo ya Taifa Letu."

Wakati Muungano huo ulioasisiwa na waliokuwa waasisi wa mataifa hayo, Hayati Mwalimu Julius Nyerere na Hayati Sheikh Abeid Amani Karume, unaadhimishwa bado makusudi ya viongozi hao yanaishi licha ya kwamba ni muda mrefu umepita. Sababu hasa za kuungana kwa iliyokuwa Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar ni kuimarisha umoja na amani miongoni mwa watu hao ambao asili yao ni wamoja na kuleta maendeleo endelevu.

Nyerere na Karume, Mungu aziweke roho zao mahali pema peponi, waliona kwamba kwa umoja baada ya mataifa hayo kujikomboa kutoka mikononi mwa watawala wa kikoloni muda mfupi, kwa kuwa taifa moja, nchi inaweza kupiga hatua katika maendeleo ya kisiasa, kijamii na kiuchumi. Waliamini kwamba umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu. Ni hakika katika miaka 60 ya Muungano, amani, umoja na mshikamano vimetamalaki ndani ya taifa la Tanzania na watu wanashirikiana katika masuala mbalimbali bila kujali maeneo wanayotoka. Kuwapo kwa Muungano kumewafanya watu kuishi pamoja na kushirikiana katika masuala mbalimbali ya kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Pia ndani ya miaka 60 ya Muungano, kumeshuhudiwa maendeleo katika nyanja mbalimbali kiuchumi na kijamii zikiwamo huduma za jamii kama vile elimu, maji, afya, miundombinu ya uchukuzi na mawasiliano.

Wakati Muungano unaasisiwa, kulikuwa na chuo kikuu kimoja tu cha Dar es Salaam ambacho wakati huo kilikuwa kishiriki cha Chuo Kikuu cha Afrika Mashariki lakini sasa kuna ongezeko kubwa la vyuo ambalo limesababisha nchi kuwa na wasomi wa kila fani. Pia shule za msingi na sekondari pamoja na vyuo vya kati na vya mafunzo ya amali vilikuwa vichache kwa wakati huo kulinganisha na sasa.

Katika afya pia, vituo vya kutolea huduma hiyo vilikuwa vichache hali ambayo ilisababisha wananchi kupata adha ya kupata tiba, hivyo kusababisha baadhi ya wananchi kupoteza maisha. Hivi sasa vituo hivyo viko hadi ngazi ya Kijiji kwa maana ya zahanati na watu wanapata huduma bila matatizo. Wataalamu wa afya pia walikuwa wachache lakini hivi sasa wako wa kutosha na serikali inaendelea kusomesha wataalamu zaidi kwa kuwa inaamini kuwa afya bora ndio msingi wa maendeleo endelevu katika nyanja zote za kimaisha.

Pia katika uchumi kumekuwa na mabadiliko makubwa kutokana na kukua kwa sekta mbalimbali za uzalishaji vikiwamo viwanda kulinganisha na hali iliyokuwa kabla na wakati wa kuanzishwa kwa Muungano. Sekta mbalimbali kama vile za fedha, utalii na viwanda zimepiga hatua, hivyo kuwezesha bidhaa mbalimbali kupatikana nchini.

Kama waswahili wasemavyo barabara ndefu haikosi kona, ndivyo ilivyo pia katika Muungano huu ambao unatimiza miaka 60. Kwa mantiki hiyo, kuna kasoro za hapa na pale ambazo zimekuwa zikijotokeza na hatua kadhaa kuchukuliwa ili kuondoa vikwazo hivyo.

Hata hivyo, kasoro kama vile tofauti za kisiasa, kiimani na kiitikadi hazijauteteresha Muungano ndiyo maana umedumu hadi sasa kwa kuwa zinasababishwa na binadamu, hivyo zinapojitokeza, pande husika zinakaa na kuzungumza na hatimaye kuzipatia ufumbuzi.

Kwa ujumla, Muungano huu una manufaa makubwa sana kwa Watanzania, hivyo hauna budi kulindwa kwa maslahi mapana ya wananchi wote. Ni imani kwamba bila Muungano hakuna umoja wala maendeleo, hivyo hauna budi kulindwa kwa nguvu zote kama mboni ya jicho.

Muungano pia unapaswa kulindwa kwa sababu zaidi ya asilimia 70 ya Watanzania kwa sasa, walizaliwa ndani ya kipindi cha miaka 60, hivyo hawajui chochote zaidi ya Muungano. Mtu yeyote atakayeibua chochochoko za kutaka kuuvunja Muungano, haitakii mema Tanzania, hivyo ashughulikiwe ipasavyo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Majibu ya kulea watoto, hadi ananyooka, mzazi ujitathmini

Na Joyce Lameck

**HALI** ya kuwa na mtoto ni hatua mojawapo ya maisha ya mwanadamu mwanzoni mwa maisha ya utoto, ndipo akili hunasa na kujifunza vitu vingi kwenye jamii, jukumu la malezi ya watoto huwa ni la baba, mama na jamii kwa ujumla.

Watoto wana haki ya kupata uangalizi na usimamizi bora kwa ajili ya maisha yao ya baadae, linahusisha kufuatilia kwa karibu maendeleo ya mtoto anapokuwa shuleni, nyumbani na jamii.

Malezi bora kwa watoto hutolewa na baba kushirikiana na mama, licha ya kuwa sasa watoto wengi hulelewa na mama pekee hii ni kutokana na sintofahamu kwenye familia nyingi katika nchi zetu.

Kinamama, wanajikuta peke yao wakilea watoto, bila kushirikiana na baba, ambao wamgewasaidia katika malezi bora, ambayo yatawasaidia kuwa na tabia njema. Ukweli ni kwamba, mama pekee kutoa malezi bora si rahisi.

Malezi ya baba kwa watoto ni msaada mkubwa, kwani sauti ya baba ni tofauti na mama. Ni sababu kubwa ya watoto kutokuwa wasikivu kwa mama zao, akiamini hana uwezo wa kumwadhibu.

Inafahamika, baba ni kichwa cha familia, mtafutaji kwa ajili ya kuhakikisha familia inapata yote muhimu wafikie kuwa na afya bora.

Hilo linawafanya kinababa wengi kusahau majukumu ya malezi kwa watoto wao na hata kuchangia kukosekana maadili bora, hata kusababisha kuing'oa katika makundi hatarishi kuongezeka kwa kasi nchini, pia idadi kubwa ya watoto wa mtaani.

Katika jamii, mama ndiye anayepewa kipaumbele katika malezi ya Watoto. Muda mwingi anakuwepo mazingira ya nyumbani utoto hauepukiki, lakini je watoto wengi wanafurahia utoto wao?

Jukumu la malezi ya watoto mara zote kwenye jamii zetu limeonekana kuwa la mama kwa asilimia kubwa lakini utandawazi, kukua kwa sayansi na teknolojia kumebadilisha hili, wanawake wengi wameingia kwenye shughuli za kujikwamua kiuchumi, muda kidogo ndio wanapatikana majumbani kulea watoto.

Malezi bora ndio chanzo cha kupata kizazi bora na chenye maadili mema. Wanapaswa kutenga muda wa kuwa karibu na watoto, ili kujenga urafiki utakaowasaidia kuwa huru kwa wazazi.

Wazazi wanapaswa kufuatilia tabia za watoto. Kumekuwapo tabia zinazoibuka kwao na baadae kuleta madhara makubwa kwa familia, hata taifa kwa ujumla.

Mzazi unapoona tabia isiyo njema ya mwanao, ni vema ukatumia njia tofauti, zitakazomsaidia mtoto kurudi katika njia sahihi. Bila ya kuweka mkazo, ni mwanzo wa kuwa wa watoto waliokosa maadili.

Msiposimama kidete katika malezi ya watoto, watajifunza vitu vibaya wanapokuwa shuleni au mazingira mengine nje na nyumbani kwani wanakutana na watu wa aina tofauti.

Pia, kwa sasa dunia inaongozwa na utandawazi, watoto wengi wanapenda kutumia vitu ambavyo vinawapeleka kwenye utandawazi kama vile simu, kompyuta na vinavyofanana navyo.

Wazazi ni vema kuweka mipaka ya uhuru kwa mtoto, katika kutumia vitu vinavyoweza kuwabadilisha maadili, hata pasipo kumsumbua mzazi.

Aidha, maendeleo ya mtoto kwenye elimu yanategemea ufuatiliaji wa mzazi. Asipotenga muda kwa ajili ya watoto, itawagharimu. Wazazi wengi wanakosa muda wa kufuatilia maendeleo ya watoto wao shuleni, wengi kuwa jukumu la mwalimu, wasaidizi wa kazi na mtoto mwenyewe.

Watoto wanaofanya vizuri kwenye elimu, ni wale wazazi wamewekeza muda katika kufuatilia maendeleo ya watoto wao shuleni. Kufuatilia maendeleo ya watoto shuleni, kunawezesha kubaini changamoto wanazokumbana nazo shuleni na kushirikiana kuzitatua kwa wakati.

Baadhi wamepitia unyanyasaji kutoka kwa walimu, majirani, wasaidizi wa kazi za nyumbani, kitu kinachochangia maendeleo duni shuleni, iwapo watakosa sehemu sahihi ya kuwasilisha tatizo lake au mtu wa kutambua mabadiliko yake kwa wakati sahihi.

Malezi bora ni mwanzo mzuri kwa watoto kukua katika maadili mema, pia kujenga kizazi bora kijacho kwa miaka ijayo, hivyo kama wazazi, walezi tunapaswa kuwajibika vema katika kutoa malezi mazuri kwa watoto.

HABARI KITAIFA

# LATRA yafafanua nauli mpya SGR

**Na Elizabeth Zaya**

MAMLAKA ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), imesema bado haijapanga nauli za Treni ya Kisasa (SGR) na kuwataka wananchi kupuuza taarifa inayosambazwa mitandaoni.

Taarifa hiyo inaonyesha viwango vya nauli inayodaiwa kwamba ndio nauli ya awali inayopendekezwa kutumika katika usafiri huo.

Katika taarifa yake kwa vyombo vya habari, Mkurugenzi Mkuu wa LATRA, Habibu Suluo, alisema taarifa hizo hazina ukweli na hivyo zinapaswa kupuuzwa.

Kadhalika, alisema kama mamlaka yenye dhamana ya kupanga nauli, bado hawajatangaza nauli zitakazotumika na kwamba nauli hizo zitatangazwa hivi karibuni na kwa sasa wapo kwenye majaribio ya mwisho.

"Kumekuwa na taarifa zinazosambaa kwa kasi zinazoonyesha nauli za awali zinazopendekezwa na Shirika la Reli Tanzania (TRC), ili kuanza kutumika katika usafiri wa reli ya SGR, sisi ni LATRA na jukumu letu ni kupanga nauli baada ya kupata maoni kutoka TRC," alisema Suluo.

"Napenda niwatoe hofu Watanzania, wenye kusambaza taarifa hizi hatujui nia yao ni nini. Kwanza siyo taarifa sahihi, na nataka niwahakikishie kwamba serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan inawajali Watanzania wa aina zote na hasa wenye hali ya chini, haitaweza kupanga nauli hizi ambazo zimesambazwa kwenye mitandao ya kijamii kwa hiyo tunaomba zipuuzwe," alisisitiza.

Suluo alisema jukumu kubwa la mamlaka hiyo pamoja na kupanga nauli, pia linatoa idhibati ya miundombinu ya reli au njia ya reli itakayotumika pamoja na idhibati ya mabehewa ambayo yatakuwa yanabeba abiria.

"Na kabla hatujatangaza nauli ni lazima tutoe idhibati ya kuanza kutumika kwa njia ya reli na pia kutoa idhibati ya kuanza kutumika kwa mabehewa. Kwa hiyo siyo muda mrefu tutatangaza nauli, majaribio yanaendelea.

"Kwa sasa hivi, abiria wale wanaosafiri ni kwa ajili ya majaribio tu siyo kwamba wanalipa nauli, hakuna nauli inayotozwa kwa sasa hivi mpaka LATRA itangaze, kwa hiyo ipuuzeni taarifa hiyo na kila mtu aendelee na shughuli zake, hatujui anayesambaza taarifa hizo ana nia gani," alisema.

# Muhongo ataka uwekezaji vyanzo vya uhakika nishati

**Na Vitus Audax,** DODOMA

MBUNGE wa Musoma Vijijini (CCM), Prof. Sospeter Muhongo, ameishauri serikali kuanzisha mchakato maalum kuanza kutumia vyanzo vya uhakika, mbadala na vikubwa vya uzalishaji nishati vitakavyolisaidia taifa kupata umeme wa kutosha.

Prof. Muhongo alitoa rai hiyo jana bungeni wakati akichangia makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Nishati kwa mwaka 2024/25 huku akibainisha kuwa nchi zilizoendelea kiuchumi na kiviwanda zimewekeza katika vyanzo vikubwa vya uzalishaji umeme vikiwamo vya jua, upepo na joto ardhi (geothermo).

"Tukianza na jua linapopiga chini unapata zaidi ya watt 342 lakini kwa nini kama Tanzania twende huku. Nimechukua mfano wa India na China ambapo kwa India mpaka mwaka huu uwezo wao kuzalisha umeme jua ni gigawatt (GW) 82 sawa ambayo ni sawa na megawati 82,000 wakiunganisha na umeme wa upepo zinafikia gigawati 609.

"Aina ya pili ni upepo mfano India wanazalisha GW 43 na wanataka ifikapo mwaka 2030 wazalishe zaidi ya GW 170 na hii tutaongea kwenye mipango tusiende na megawati kidogokidoga lazima tuwe na mpango wa uzalishaji mkubwa,"alisema Prof. Muhongo.

Pia alisema China kupitia upepo wanazalisha GW 440 na ifikapo 2030 wanatarajia kuzalisha umeme kupitia upepo na jua GW 1,300 sawa na Megawatt milioni 1.3, hivyo si ajabu Tanzania kwenda kununua vitu India na China kwa sababu umeme wao ni wa viwanda.

Kwa Afrika, alitolea mfano wa Kenya ambayo inaongoza kwa uzalishaji wa umeme mwingi. Alisema nchi hiyo inazalisha MW 440 katika Ziwa Trukana pamoja na umeme wa jotoardhi kwenye bonde lao la ufa MW 981.

Alisema zamani Tanzania ilikuwa ikizidi Kenya kwa uzalishaji wa umeme lakini kwa sasa umeme wao kwa ujumla ni MW 3300 sawa na GW 3.3 kulinganisha na Tanzania inayozalisha MW 2,138.

Aliiomba serikali kutumia ramani iliyotengenezwa ikibainisha maeneo yanayoweza kuzalisha umeme jua kwa wingi zaidi yakiongozwa na Shinyanga ili kupata umeme wa kutosha kupitia jua pamoja na vyanzo vingine ili kufikia MW 10,000 zitakazosaidia katika uendeshaji viwanda kwaajili ya maendeleo.

Mbunge wa Geita Mjini (CCM), Ally Makoa, aliitaka serikali kurejea vijijini na kuangalia katika maeneo mengi ambayo hayajafikiwa na umeme licha ya kutajwa kwa vijiji husika kuwa vimefikiwa na huduma hiyo.

Alisema licha ya serikali kutekeleza miradi hiyo katikma maeneo husika wakandarasi wanashidwa kufikia malengo, kwani wanaomba umeme ni wengi lakini unawafikia watu wachache kutokana na uwezo mdogo wa usambazaji.


IITA
Transforming African Agriculture CGIAR

## POSITION ANNOUNCEMENT

### RESEARCH ASSOCIATE

### IITA-TZ-2024-NRS-003-NRS-ARUSHA

The International Institute of Tropical Agriculture (IITA) is a not-for-profit institution that generates agricultural innovations to meet Africa's most pressing challenges of hunger, malnutrition, poverty, and natural resource degradation. Working with various partners across sub-Saharan Africa, we improve livelihoods, enhance food and nutrition security, increase employment, and preserve natural resource integrity. IITA is a member of CGIAR, a global agriculture research partnership for a food secure future.

IITA is looking for a suitably qualified person to fill the positions of Research Associate to support the IITA banana project based at the IITA Office at the Nelson Mandela African Institution of Science and Technology (NMAIST) in Kijenge, Arusha.

**Responsibilities:**

- Work with representatives of the national programs of Tanzania and Uganda to design and implement consumer preference analysis of new banana hybrids.
- Conduct consumer preference panels, interacting with farmers to obtain rele vant input to guide.
- Conduct phenotyping of banana colour and texture.
- Oversee collection of data related to quality of banana.
- Prepare reports and ensure timely delivery as required by supervisor.
- Describe banana varieties using characterization variables.
- Assist administration for import and export of plant material.
- Carry out any other responsibility as may be assigned by the supervisor.

**Required Qualifications / Experience**

- MSc in Plant Breeding, Food Science or related field.
- Ability to work independently with minimal supervision, but also participate as a team member in accom plishment of duties.
- Experience in statistical analysis.
- Possess excellent interpersonal and communication skills in English.
- Have experience in conducting Agricultural surveys.
- Knowledge or experience related to gender, diversity and inclusion.
- Food quality evaluation skills

The initial contract for the position is for Six month: Renewable subject to performance and availability of funds. The duty station for the position will be IITA in Arusha. This is a nationally recruited position and IITA offers a competitive remuneration package.

**Applications:** Applications including curriculum vitae, copies of certificates, telephone number, email address, and names and addresses of two referees should be sent to the Country Representative, IITA-Tanzania, Plot No. 25, Mwenge – Coca-Cola Road, Mikocheni Industrial Area P.O. Box 34441, Dar es Salaam, Tanzania or by email to **IITA-Tanzania@cgiar.org**

Applicants are requested to please indicate the reference number for the position as indicated on the heading of the announcement in your application as well as on the subject of your email if sending by email. If sending by post or hand delivery, please indicate the reference number on your application as well as on the left-hand side of your envelope. Please note that any applications without the reference indicated will be automatically disqualified.

**Closing date:** Two weeks from the date of advertisement appearing in the newspaper. Please note that only shortlisted candidates will be contacted.

# Mamalishe wanolewa kukabili majanga ya moto

**Na Mwandishi Wetu,**
ARUSHA

KAMPUNI ya Geita Gold Mining Limited (GGML) kwa kushirikiana na Wakala wa Usalama na Afya Mahala pa Kazi (OSHA) wametoa mafunzo maalum kwa mamalishe 50 wa Mkoa wa Arusha kwa lengo la kuwaelimisha namna ya kukabiliana na majanga ya moto.

GGML pia imegawa mitungi 50 ya gesi ya kupikia kwa kundi hilo ili kuhamasisha kinamama hao kuachana na matumizi ya kuni na mkaa na kuhamia kwenye matumizi ya nishati safi.

Mafunzo hayo yalitolewa jana Jumatano katika maadhimisho ya Kimataifa ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi yanayofanyika Kitaifa jijini Arusha kuanzia Aprili 23 hadi Mei Mosi mwaka huu.

Meneja Mwandamizi wa Afya, Usalama na Mazingira kutoka GGML, Dk. Kiva Mvungi, akizungumza na mamalishe hao, alisema wameamua kutoa elimu kwa kinamama hao ili watambue namna ya kupambana na moto majumbani na kuzingatia usalama kwenye maeneo yao ya biashara hasa ikizingatiwa wao hukutana na watu wengi.

"Tunawafundisha namna ya kupambana na majanga ya moto kwani shughuli zao za kila siku zinahusiana na masuala ya moto na matumizi ya mkaa na gesi.

"Lakini pia ni vyema kutambua namna gani mabadiliko ya tabianchi yanaathiri watu pia namna tabia zetu binafsi zinavyoweza kuchangia kuachana na ukataji ovyo wa miti," alisema.

Aliongeza kuwa athari za mabadiliko ya tabianchi ziko kwa kila mmoja bila kujali cheo, mkubwa au mdogo, hivyo ni vyema kila mmoja kuzingatia matumizi ya nishati safi ili kuondokana na majanga yatokanayo na mabadiliko hayo.

"Tumeandaa elimu hii kuona namna ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kwa sababu ukataji miti ukikithiri unasababisha mmonyoko wa ardhi, mafuriko na ongezeko la joto duniani.

"Matumizi ya mkaa au kuharibu vyanzo mbalimbali ambavyo vinaweza kusababababisha athari kwenye mazingira na kusababisha mafuriko hata kwenye maeneo yetu ya uchimbaji," alisema.

Ofisa Mwandamizi wa Masuala ya Jamii na Maendeleo ya Kiuchumi kutoka GGML, Ruth Mharagi alisema katika mafunzo hayo, wamefundisha kinamama hao namna salama ya kutumia nishati ya gesi na kusisitiza kuondokana na matumizi ya mkaa.

"Lakini pia kwenye banda letu tumeendelea kupokea wageni wanaopenda kujifunza namna ya kupambana na majanga ya moto kwa sababu asilimia kubwa wana uelewa mdogo namna ya kukabiliana na majanga ya moto majumbani.

"Watu wengi hawajui njia za awali za kupata msaada wa kuzima moto, sisi tunatoa mafunzo hayo, kuna vifaa vya kawaida ambavyo mama yeyote anavyo nyumbani, mfano ndoo ya maji, taulo, kanga au kitenge vilivyolowekwa kwenye maji, ni vifaa vya kawaida ambavyo unaweza kutumia kuzima moto hivyo tunaendelea kuwaakaribisha kwenye mabanda yetu," alisema.

Mkaguzi wa Afya ya Mazingira ya Kazi kutoka OSHA, Elizabeth Mtile alisisitiza kinamama hao kuzingatia umuhimu wa kufuata sheria na miongozo mbalimbali ya usalama na afya katika maeneo ya kazi.

"Kaulimbiu yetu inayosema athari za mabadiliko ya tabianchi katika usalama na afya kazini, inalenga kudhibiti majanga na mabadiliko haya ya tabianchi kwa kushirikisha kila kundi kwenye jamii kwani athari hizi zinatugusa sote," alisema.

Mmoja wa mamalishe hao, Prinsila Kwai aliishukuru GGML na OSHA kwa kupatia mafunzo hayo, akiamini yanakwenda kuwa chachu ya mabadiliko kwao na kwa wale wanaowazunguka.

"Kwa kweli tunashukuru sana kwa shughuli zetu za kila siku zinahusiana na moto, hivyo mafunzo haya yatatusaidia sana namna ya kukabiliana na mlipuko kama vile wa gesi," alisema.



Mkuu wa Shule ya Polisi Tanzania - Moshi, SACP Ramadhani Mungi (wa pili kulia), akipokea msaada wa seti ya vitanda kutoka kwa Mkuu wa Kitengo cha Masoko wa Benki ya Exim, Stanley Kafu, shuleni hapo, mjini Moshi mkoani Kilimanjaro juzi, ikiwa ni sehemu ya mchango wa benki hiyo, katika utoaji wa huduma kwa jamii ikiwemo ulinzi na usalama wa raia na mali zake. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# DIT yaanza kuwalinda wabunifu

**Na Joseph Mwendapole**

TAASISI ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT), imeanzisha utaratibu wa kuwapa mafunzo ya ubunifu walimu na wanafunzi wabunifu wa taasisi hiyo ili wawe na uwezo wa kulinda ubunifu wao.

Mafunzo hayo yatawawezesha kupata cheti cha umiliki wa ubunifu wao kitakachotolewa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA).

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi wa Utafiti, Ushauri wa Kitaalam na machapisho, Dk. Respicius Kiiza wa taasisi hiyo, wakati akifungua mafunzo ya siku tano kwa wabunifu hao.

Alisema Taasisi imeona umuhimu wa kuwapatia utaalamu wabunifu wote kuhusu namna ya kulinda bunifu zao na iko tayari kuzigharamia kwa ajili ya matumizi ya kibiashara.

"Kufanya bunifu kibiashara ni hatua kubwa na ukiwa na bunifu yako inakuwa na chapa hivyo basi mafunzo haya yawe chachu kwa wabunifu wote na mjitahidi kuhudhuria mafunzo ili mwisho wa siku kila mmoja aweze kujihakikishia kuwa anaweza kuandaa nyaraka inayoweza kutumika kulinda bunifu yake," alisema Dk. Kiiza.

Naye Mratibu wa Ubunifu, Utafiti na Machapisho wa DIT, Dk. Daudi Simbeye, alisema nia ya DIT ni kuwawezesha wabunifu kulinda kazi zao na kuzifanya kibiashara zaidi.

Alisema DIT imejikita zaidi katika kutatua changamoto za jamii na kwamba Taasisi hiyo ina bunifu nyingi ambazo hazina ulinzi wa kisheria hivyo DIT imeamua kutoa mafunzo kwa lengo la kuwapa uwezo walimu na wanafunzi ili waweze kusajili bunifu zao.

"Wabunifu wetu wana kazi nzuri sana ambazo zimeshiriki kwenye maonesho ya ndani na nje ya nchi na zimefanya vizuri sana na kupatia Taasisi ushindi lakini sasa bunifu hizi zilikuwa hazina ulinzi jambo ambalo lilikuwa linatuogopesha," alisema.

Aidha, alisema bila ulinzi bunifu hizo zinaweza kuibiwa hivyo baada ya mafunzo hayo ya siku tano wana uhakika wa kulinda bunifu zao na watazitumia kibiashara zaidi.

Mafunzo hayo ya siku tano yanahudhuriwa na washiriki (50) na yanatolewa na watalaam kutoka (BRELA).

# Takukuru yabaini ubadhirifu katika ujenzi barabara

**Na Julieth Mkireri,**
KIBAHA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Pwani, imesema imebaini kuwepo kwa dalili za ubadhirifu mradi wa ujenzi wa barabara ya Picha ya Ndege - Boko Timiza inayojengwa na Wakala wa Barabara Mjini na Vijijini (TARURA).

Kwa mujibu wa TAKUKURU, dalili hizo zimebainika kutokana na mradi huo ambao ulipaswa kujengwa kilometa moja kwa gharama ya Sh. 943,500,600 lakini imejegwa mita 700 pekee.

Akizungumza na waandishi wa habari jana mjini hapa kuhusiana na taarifa ya miezi mitatu ya taasisi hiyo, Naibu Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Pwani, Ally Sadiki, alisema barabara hiyo ilipaswa kujengwa kwa urefu wa kilometa moja lakini imejegwa kwa mitaa 700.

Sadiki alisema taasisi hiyo imebaini kuwapo kwa harufu ya ubadhilifu katika mradi huo ambao unajengwa kwa kiwango cha lami na Globalink General Contractors Ltd.

Naibu mkuu huyo alisema baada ya kubaini kuwapo kwa hali hiyo waliofanya mahojiano na baadhi ya viongozi wa TARURA ambapo waliagizwa kuhakikisha mradi huo unatekelezwa kikamilifu kama ilivyopangwa.

Sadiki alisema kutokana na kubaini uwepo wa uovu katika mradi huo wanaendelea na taratibu nyingine na zikikamilika hatua za kisheria zitachukuliwa kwa wahusika

Pia alisema taasisi hiyo imefanya ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo 23 yenye thamani za Sh. bilioni 6.3, ikiwamo ya elimu, maji, afya na miundombinu na kwamba kasoro zilizobainika zimetafutiwa ufumbuzi.

Alisema taasisi hiyo imejiwekea mikakati mbalimbali ikiwamo kuendelea kudhibiti mapato ya serikali na usimamizi wa rasilmali za umma samabamba na kuwachukulia hatua za kisheria watumishi na viongozi watakaobainika kufuja mali hizo.

# MIAKA 60 YA MUUNGANO



**YALIYOMO**



**Prof.Kabudi achanganua mzizi wake, Nyerere na Karume...'Kazi iendelee'**

UKURASA 10



**TANESCO, ZECO zabadilishana uzoefu kutatua changamoto nishati**

UKURASA 11

# Prof. Kabudi achanganua mzizi wake, Nyerere na Karume... 'Kazi Iendelee'

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SIRI ya Kudumu kwa miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar tangu ulipoasisiwa mwaka 1964, imetajwa kuwa ni ridhaa zinazotokana na mapenzi na undugu wa muda mrefu wa wananchi wa pande mbili hizo.

Mwanazuoni wa Sheria kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ambaye sasa ni Mbunge wa Kilosa, Profesa Palamagamba Kabudi, anasema muungano huuma katika misingi ya umoja, ushirikiano na mapenzi ya kihistoria na damu, usio na unasaba na mapigano.

Profesa Kabudi anaufafanua kuwa, unaacha viashiria kwamba, kuna mwingiliano wa muda mrefu yakihusishwa na harakati za ukombozi kutoka kwenye ukoloni.

Anataja kuwapo, mchanganyiko wa makabila ya Zanzibar katika miaka ya 1945, wakati wa ukoloni pamoja na biashara ya utumwa, yalichagiza kwa kiasi kikubwa kujenga uhusiano wa leo.

Msomi huyo anawataja viongozi, Mwalimu Julius Nyerere na Mzee Abeid Karume, walishirikiana katika harakati za uhuru, wakipanga mbinu na safari zao zilikuwa za pamoja.

Hapo anarejea safari za viongozi hao kwenda Lancaster, Uingereza kuichagiza uhuru wa nchi, pia Accra -Ghana kulikofanyika mikutano mikubwa ya nchi za Afrika kupewa mbinu za kudai uhuru, baada ya Ghana kupata uhuru mapema mwaka 1957 kutoka kwa Uingereza.

"Hapo ndipo mahusiano makubwa ya viongozi wa vyama vilivyokuwa katika harakati za kupigania uhuru, hayati Karume na Nyerere yalipoanza. Walishirikiana kikamilifu katika kudai uhuru pamoja na kufanya safari za pamoja" anaeleza msomi huyo. Anatoa mfano, baadhi ya mataifa ya Afrika yalijaribu kuunganisha nchi zao lakini bila ya mafanikio, baadaye muungano wao ulivunjika katika kipindi kifupi.

Katika hilo, anazitaja nchi ya Ghana, Guinea na Mali zilishindwa kuungana, licha ya juhudi za viongozi waasisi katika uhuru wa Afrika, akifafanua:.

"Viongozi waasisi wa uhuru wa Bara la Afrika ikiwemo Sekou Toure wa Guinea, Kwame Nkrumah wa Ghana pamoja na Modibo Keita (Mali), muungano wa nchi hizo tatu ulivunjika."

Aidha, anautaja Muungano wa Misri pamoja na nchi ya Kiarabu ya Syria uliofahamika kwa jina la United Arab Republic UAE uliofanyika Februari 1, 1958 ulivunjika na mwingine ni wa Senegal na Gambia, nazo zilidumu kwa miaka minane tu, kuanzia mwaka 1982 hadi 1989.



Profesa Palamagamba Kabudi. **PICHA ZOTE: MAKTABA**

Professa Kabudi anataja sababu za kuvunjika muungano huo, ilikosa ridhaa za wananchi wake, wanaotofautiana kwa mengi, ikiwamo ujirani mwema.

**SHAMSI VUAI NAHODHA**

Aliyekuwa Waziri Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), Shamsi Vuai Nahodha, anautaja muungano kuwa tunu ya taifa na unapaswa kuenziwa, huku vijana wakabidhiwe jukumu la kuurithi, kwani waasisi na wazee wameshaziunganisha nchi hizo.

Shamsi anampongeza Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kwa kuonyesha nia katika kuzipatia ufumbuzi changamoto zake.

Anamtaja Rais Dk. Samia, yu msikivu na kiongozi aliyefahamu vyema changamoto zake ikizingatiwa alishatumika kuwa, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, anayeshughulikia Muungano, baadaye akawa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano.

Waziri wa SMZ Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Dk. Sada Mkuya Salum, anasema Zanzibar inaridhishwa na inavyoshirikishwa katika masuala ya kifedha na taasisi katika vyombo vya kimataifa vya fedha, ikiwamo Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF).

Anasema, Zanzibar kukua kimaendeleo, inategemea zaidi mafanikio makubwa katika masuala ya fedha na ukuaji Uchumi, inategemea sana ushirikishwaji katika vyombo vya kimataifa vya fedha, vinavyoamua masuala ya sera na uchumi.

Dk. Saada anasema, Zanzibar inanufaika na ushauri wa kifedha unaotolewa na Benki Kuu ya Tanzania (BOT), katika masuala ya kisera na fedha.

Anataja zao la ushirikishwaji wa Zanzibrav, umeleta mageuzi yatokanayo na marekebisho makubwa Kimuungano, pia mazungumzo kuhusu Zanzibar na ushirikishwaji wake katika masuala ya mikopo kutoka taasisi za fedha za kimataifa,



Mwalimu Julius Nyerere na Mzee Abeid Aman Karume, wakitia saini hati za Muungano.

MIAKA 60 YA MUUNGANO

# TANESCO, ZECO zabadilishana uzoefu kutatua changamoto nishati

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

WAKATI mwaka huu Tanzania ikiadhimisha miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar moja ya maeneo ambayo yamenufaika na muungano huo ni sekta ya nishati ambayo nchi zote mbili kupitia mashirika yote mawili ya umeme ya Zanzibar (ZECO) pamoja na upande wa bara (TANESCO) zimekuwa na ushirikiano mkubwa kwenye kubadilishana uzoefu pamoja na kushirikiana kutatua changamoto mbalimbali.

Kwa kuthibitisha hilo hivi karibuni Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) na Shirika la Ugavi na Usambazaji Umeme Tanzania (TANESCO) wameanza mchakato wa uwekaji wa njia mpya ya usafirishaji umeme katika kisiwa cha Unguja, Pemba na Mafia.

Ripoti ya awali ya upembuzi yakinifu iliyofanywa na kampuni ya CESI, ELC na COLENCO Aprili 22, 2024 imebainisha kuwa ipo haja ya kuweka nyaya nyingine zenye uwezo mkubwa kutokana na ongezeko kubwa la matumizi ya umeme katika visiwa hivyo.




Mkurugenzi wa Tanesco Eng. Gissima Nyamo-Hanga

Unguja imeunganishwa na meme wa Gridi ya Taifa kutoka kituo cha Tegeta Tanzania Bara kwa njia ya awali yenye uwezo wa kubeba megawati 45 na kusafirisha umeme wa msongo wa kilovolti 132, na njia ya pili ya waya wenye uwezo wa kubeba megawati 100 na kusafirisha umeme wa msongo wa kilovolti 132.

Aidha, Pemba imeunganishwa na kituo cha umeme cha Majani Mapana, Tanga kupitia waya wenye uwezo wa kubeba megawati 20MW na kusafirisha umeme wa msongo wa kilovolti 33.

Katika harakati za kuongeza upatikanaji wa umeme visiwani Zanzibar njia mpya za usafirishaji umeme zinakusudiwa kujengwa ambapo Unguja njia ya msongo wa kilovolti 220 yenye uwezo wa kubeba megawati 200, Pemba kutawekwa njia ya msongo wa kilovolti 132, yenye uwezo wa kubeba megawati 100.

Mbali na uwekaji wa njia hizo, pia mradi huu unakusudia kujenga vituo vya kusafirishia na kupoozea umeme katika visiwa vyote hivyo.



Sample ya laini ya msongo wa Kilovoti 220.

Mradi huu unafadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kupitia Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

Lakini pia katika kubadilishana uzoefu Bodi ya Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) imekuwa ikifanya ziara mbalimbali za kujifunza katika mikoa ya Tanzania bara ikiwemo ziara ya kutembelea miundombinu ya uzalishaji umeme mkoa wa Kigoma kujifunza namna ya uzalishaji umeme.

Pia, ushirikiano mwingine ni kuanza kwa mchakato wa kuongeza laini ya kutoka Kunduchi mpaka Mtoni Zanzibar itakayopitisha Megawati 200 za umeme.

ZECO ni moja ya wateja wakubwa na muhimu kwa TANESCO ikitajwa kuchangia sehemu kubwa ya mapato ya TANESCO kiasi cha takribani shilingi bilioni 91.7 za kitanzania kwa mwaka.

Katika kuendelea na jitihada za kuongeza vyanzo vya uzalishaji umeme kuendana na juhudi za Serikali ya Zanzibar TANESCO na ZECO zimeanza mchakato wa haraka wa kuongeza laini nyingine (marine cable) kutoka Kunduchi mpaka Mtoni Zanzibar itakayopitisha megawati 200.

Ifahamike kwamba juhudi za kuendelea kuipatia Zanzibar umeme wa uhakika zilifanyika katika kila awamu katika utekelezaji wa wajibu huo.

Na sasa ni miaka 60 ya mafanikio makubwa ambapo TANESCO wamefanikiwa kusambaza umeme visiwani Zanzibar na kuwezesha ZECO kuwaunganishia umeme takribani wananchi 93,124.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Hussein Ali Mwinyi katika hotuba yake ya miaka 60 ya Mapinduzi mapema mwaka huu alisema katika awamu zote baada ya Mapinduzi, Serikali ilifanya jitihada za kuwezesha upatikanaji wa huduma za umeme kwa wananchi pamoja na miradi ya kiuchumi.

"Tunapoadhimisha miaka mitatu ya Serikali ya Awamu ya Nane, mafanikio yamepatikana katika kuimarisha upatikanaji wa huduma za umeme nchini.

Alisema kwa lengo la kuhakikisha wananchi wanapata huduma za umeme kwa urahisi, Serikali imepunguza bei ya kuunganisha umeme kwa wananchi kwa wastani wa asilimia 50.

Alisema hatua hiyo imesababisha idadi ya wateja wanaoomba kuunganishiwa umeme kuongezeka hadi kufikia wastani wa wateja 200 kwa siku katika kipindi hiki kutoka wastani wa wateja 50 kwa siku hapo awali.

"Wananchi wengi wameweza kufikiwa na huduma ya umeme ambapo Shirika la ZECO limeweza kuwaungia umeme wananchi 93,124; (Unguja 78,122 na Pemba 15,002) sawa na ongezeko la wateja kwa asilimia 45 kwa kipindi cha miaka mitatu.

Alisema katika kuhakikisha Zanzibar inapata vyanzo vyake vya ndani vya uzalishaji umeme, Serikali imesaini mkataba wa mauziano ya umeme (PPA) na Kampuni ya Generation Capital Ltd kwa lengo la kuwekeza katika nishati ya umeme wa jua kwa kujenga mtambo wenye uwezo wa kuzalisha megawati 130.

Aidha, Serikali imetiliana saini na Kampuni ya ESR ya Ujerumani ambayo itazalisha megawati 15 za umeme wa jua kwa ajili ya kisiwa cha Pemba.

Sambamba na hatua hiyo, Serikali inashirikiana na mshauri elelezi kutoka Kampuni ya NOVAVIS INTERNATIONAL ya Marekani kufanya upembuzi yakinifu wa kutafuta ufumbuzi wa changamoto ya umeme mdogo katika baadhi ya maeneo hapa nchini.

Vile vile, mshauri elekezi wa Kampuni ya WSP ya Canada amepatikana kwa ajili ya upembuzi yakinifu wa mradi wa ujenzi wa laini kubwa ya kilowati 132 ya Mkoa wa Kusini na Kaskazini Pemba kwa ufadhili wa AfDB, KOICA na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO).

Kwa kutambua umuhimu wa ushirikiano wa TANESCO na ZECO hati ya makubaliano (MOU) kati ya Wizara ya Nishati ya Tanzania Bara na Wizara ya Maji, Nishati na Madini ya Zanzibar ilisainiwa ambapo makubaliano ya kuimarisha ushirikiano katika sekta ya nishati yalifanyika Tarehe 12 Novemba 2023 ili kuendeleza ushirikiano katika masuala ya nishati ikiwemo uzalishaji wa umeme, usafirishaji, usambazaji, uendeshaji, matengenezo, msaada wa kiufundi, mafunzo na kujengeana uwezo.

Wakati tunapo sherehekea miaka 60 ya Muungano, Ushirikiano wa TANESCO na ZECO utaendelea kuwa muhimu katika kuimarisha upatikanaji wa huduma ya umeme, kuchochea uchumi wa Viwanda na utekelezaji mikakati ya kuwa na nishati ya umeme endelevu, tukiwa pamoja, tukiimarisha Muungano wetu na kuangaza maisha kwa kila Mtanzania.



Kituo cha kupoza na kusambaza umeme.



Kituo Cha kupokea na kupoza umeme cha Majani Mapana, ambacho pia kinatumika kusambaza umeme kwenye baadhi ya maeneo ya Zanzibar.

# WASTAAFU WAENDELEA KUNUFAIKA NA MAFAO BORA YATOKANAYO NA UWEPO WA NSSF IMARA NA ENDELEVU



Masha Mshomba
**Mkurugenzi Mkuu, NSSF**




- Wazee ni kundi muhimu katika jamii yetu lililobeba uzoefu mkubwa, ujuzi, busara, taswira na kumbukumbu ya mambo mbalimbali.



Mwanachama wa NSSF akipata huduma

**Na MWANDISHI WETU**

Kwa kutambua umuhimu wa wazee na mchango wao katika jamii, Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) unatoa mafao ya pensheni ya uzee ambayo hulipwa kila mwezi kwa mwanachama aliyetimiza sifa ili yaweze kumuhifadhi kipindi chote ambacho hana uwezo wa kufanya shughuli za uzalishaji mali kutokana na umri.

Bw. Masha Mshomba, Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, anaeleza kwamba pensheni ya uzee ni mojawapo ya mafao saba (7) yanayotolewa na NSSF. Mafao hayo hulipwa kwa mwanachama aliyetimiza umri wa kustaafu kwa hiari kuanzia miaka 55 mpaka 59 au kustaafu kwa lazima kwa umri wa miaka 60 na ambaye huwa amechangia kwenye Mfuko mpaka kustaafu kwa kipindi kisichopungua miezi 180 sawa na miaka 15.

**Je, pensheni ya uzee imegawanyika katika mafungu mangapi?**

Bw. Mshomba anasema pensheni ya uzee ipo katika mafungu mawili. Kwenye fungu la kwanza, mstaafu hulipwa mkupuo wa awali ambao watu wengi wamezoea kuuita kiinua mgongo na fungu la pili ni pensheni ya kila mwezi.

**Je, ikiwa mwanachama amekidhi vigezo vya kulipwa pensheni ya uzee anatakiwa kufanya nini ili aweze kulipwa mafao hayo?**

Ndugu James Oigo ni Meneja Usimamizi Mafao wa NSSF, anasema mwanachama aliyekidhi vigezo vya kulipwa pensheni ya uzee kwa kustaafu kwa hiari au kwa lazima na akiwa amechangia NSSF kwa muda usiopungua miezi 180 sawa na miaka 15 anatakiwa kufanya mambo yafuatayo:

- **Moja;**

Kupata barua kutoka kwa mwajiri wake inayoonesha kuwa ajira yake imefika kikomo kwa kufikisha umri wa miaka 60 au kuomba kustaafu kwa hiari na mwajiri ameridhia na amempa barua ya kustaafu.

- **Mbili;**

Baada ya kupata barua ya kustaafu, Mwanachama anatakiwa kuwasilisha katika ofisi za NSSF nakala ya barua yake ya kustaafu, akiambatanisha nakala ya kadi ya uanachama wa NSSF, kitambulisho cha Taifa (NIDA) au namba ya NIDA au Kitambulisho cha mpiga kura kwa wale wasio na NIDA pamoja na picha tatu ndogo za passpot saizi.

- **Tatu;**

Anatakiwa pia kuwasilisha taarifa za akaunti ya benki kwa sababu malipo yanafanyika moja kwa moja kwenye akaunti za wanachama kupitia benki zao.

- **Nne;**

Mwanachama atajaza fomu maalum ya madai ya pensheni ya uzee akiambatanisha nyaraka zilizoainishwa hapo juu. Baada ya kujaza fomu ya madai, jalada litafunguliwa na mwanachama atalipwa ndani ya siku 30.

**Je ni vitu gani vinavyojenga pensheni?**

Ndugu Oigo anasema pensheni inajengwa na vitu viwili vikubwa ambavyo ni *"muda mtu aliofanya kazi na kuchangia kwenye Mfuko wa Pensheni pamoja na wastani wa mishahara bora ya miaka mitatu katika kipindi cha miaka kumi (10) ya mwisho ya utumishi wa mwanachama".*

**Je ni kwa nini wakati mwingine, watu waliostaafu pamoja wakiwa na mshahara unaolingana na cheo kimoja, wanatofautiana viwango vya pensheni?**

Majibu ya maswali hayo yanatolewa na ndugu James Oigo ambaye anasema kuwa *"tofauti ya vipindi vya uchangiaji ndio husababisha viwango vya pensheni viwe tofauti kwa watu waliostaafu wakiwa na cheo kimoja na mshahara unaofanana".*

Kwa mfano aliyefanya kazi kwa muda wa miaka 15 sawa na miezi 180 atapata kiwango cha pensheni tofauti na aliyefanya kazi kwa muda wa miaka 30 sawa na miezi 360 japokuwa wamestaafu pamoja wakiwa na mshahara unaofanana.

**Je baada ya kustaafu kazi ulichukua muda gani kulipwa mafao yako?**

Mzee Ibrahim Mwasili, mkazi wa Dar es Salaam, anashuhudia kuwa baada ya kustaafau alipata mafao yake kutoka NSSF ndani ya mwezi mmoja.

"Naishukuru sana NSSF kwa kuweza kunifikisha mpaka hapa nilipo na bado naendelea kupata mafao ya kila mwezi na naishi vizuri sana," anasema Mzee Mwasili.







Mwanachama wa NSSF akihakiki taarifa zake

# Pata picha ya Muungano ulivyo




**Na Mwandishi Wetu**

JAMHURI ya Muungano wa Tanzania iliundwa tarehe 26 Aprili 1964, ikiwa ni Muungano wa Mataifa mawili huru ya Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar, yaliyoingia mkataba wa Muungano mnamo mwaka 1964 na kuanzishwa Dola ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mkataba wa Muungano ulitiwa saini na aliyekuwa Rais wa Tanganyika, Hayati Mwalimu Julius Nyerere na aliyekuwa Rais wa Zanzibar, Hayati Sheikh Abeid Amani Karume mnamo tarehe 22 Aprili 1964 huko Zanzibar. Mkataba huo ulithibitishwa na Bunge la Tanganyika na Baraza la Mapinduzi hapo tarehe 26 Aprili 1964.

Tarehe 27 Aprili 1964 viongozi wa nchi zote mbili walikutana katika ukumbi wa Karimjee jijini Dar es Salaam na kubadilishana Hati za Muungano.

Sheria za Muungano zilitoa tamko la Jamhuri ya Muungano "Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar zitalazimika, baada ya kuungana na siku zote baada ya kuungana, kuunganishwa kuwa Dola ya Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Jina jipya ikawa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kupitia Sheria ya Jamhuri ya Muungano, mwaka 1964.

Itakumbukwa tendo ambalo lilifanyika siku hiyo ambapo Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alichanganya udongo wa Tanganyika na Zanzibar ikiwa ni ishara ya kuunganisha nchi mbili wakati wa Sherehe ya Muungano Dar es Salaam mnamo tarehe 26 Aprili 1964

### MUUNDO WAKE

Kwa kutazama muundo wa Muungano wa Tanzania kama ulivyoelezwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, una vyombo viwili vyenye mamlaka ya utendaji ambavyo ni Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Vyombo viwili vyenye mamlaka ya kutekeleza utoaji haki ambavyo ni Mahakama ya Jamhuri ya Muungano na Mahakama ya Zanzibar; na vyombo viwili vyenye mamlaka ya kutunga sheria na kusimamia utekelezaji wa shughuli za umma ambavyo ni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inashughulikia yote ya Muungano kama yalivyoainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na yasiyo ya Muungano kwa upande wa Tanzania Bara.

Aidha, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inashughulikia mambo yote yasiyo ya Muungano kwa upande wa Tanzania Zanzibar.

### SABABU YA KUWAPO

Muungano wa Tanganyika na Zanzibar umekuwepo kutokana na sababu mbalimbali kama vile Uhusiano wa karibu na wa kihistoria baina ya Tanganyika na Zanzibar katika nyanja mbalimbali kama vile udugu wa damu, biashara, utamaduni, lugha na mahusiano ya karibu kisiasa hususan baina ya vyama vya TANU na ASP.

Pia, azma ya kuwa na Muungano wa Afrika hususan kwa kuanzia na Shirikisho la Afrika Mashariki. Hata kabla ya uhuru wa Tanganyika, Mwalimu Nyerere pamoja na viongozi wengine waliokuwa wakipigania uhuru katika ukanda wa Afrika walikuwa na matarajio ya kuwa na Muungano wa Afrika. Mwalimu Nyerere binafsi alipendelea uwepo wa Muungano wa Afrika kwa kuanzia na Mashirikisho ya kikanda. Kimsingi, zipo sababu mbalimbali zilizosababisha Muungano huu kama vile historia za nchi hizi mbili, ukaribu wa nchi hizi mbili, muingiliano wa kijamii, ushirikiano wa kibiashara, ushirikiano madhubuti na wa muda mrefu wa kisiasa baina ya TANU na ASP, ushirikiano na urafiki wa muda mrefu kati ya watu, viongozi, na wakati wa harakati za utaifa uliopelekea uhuru wa nchi hizo mbili.




# Dk. Samia Awamu ya Sita, Dk. Mwinyi Awamu ya Nane wang'ara nao kivyao

• Waliozaliwa nao, mwaka huu wanastaafu



Rais Samia Suluhu Hassan, akiwa na mwenyeji wake, Dk. Hussein Mwinyi, Rais wa Serkali ya Mapinduzi Zanzibar, Ikulu ya Zanzibar. **PICHA: MAKTABA**

**Na Peter Orwa**

LEO Watanzania wanasherehekea miaka 60 ya Muungano. Si haba, taifa la Ghana na majirani zake walijaribu, wakashindwa, kama ilivyo kwa Misri na majirani wake Uarabuni.

Kuna usemi usione vyaelea vimeundwa. Miaka 60 ya Muungano viashiria gani vinavyoudumisha kwa zaidi ya nusu karne? Waliozaliwa mwaka huo wa Muungano, mwaka huu wanastaafu kazi kuanza kufuatilia kikokotoo chao.

Wasomi wa taaluma sayansi ya siasa kama vile Mwingereza David Easton na Mmarekani Harold Laswel, wanataja siasa kufanikiwa inahitaji suala kukubalika kwa waendeshaji wake. Ni 'legitimacy' wanavyoita wenyewe.

Leo hii hao waliojaribu kuagana 'wakachemka' kwa pamoja walikwamishwa na hilohilo la dhana 'kukubalika' kwa wananchi wake. Zote zilidumu chini ya miaka 10 zikavunjika.

Kukubalika huko huwa kuna mizizi yake kama ilivyo penye elimu, unaanzia katika; Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK), wahandisi ujenzi wao wanadumu katika 'Structural Engineering' yaani utaalamu katika msingi wa jengo.

Hapo daktari wa kutibu binadamu, fani yao wanaanza na kusoma mwaka wa kwanza katika somo liitwalo 'anatomy and physiology', ambalo linachambua mwili wa binadamu na kazi zake, kisha anasukwa katika namna ya kuutibu.

Anayesomea ugavi na ununuzi, wenyewe sasa wanaiita 'Suply Chain Management' wana kinachoitwa '5Rs (five rights)'. Ili utimie katika fani hiyo, lazima uzingatie hizo 'R' tano; Idadi sahihi ya unachohitaji (Quantity), Ubora (Quality), bei, chanzo (source) na muda sahihi.

Mwanahabari katika dodosa zake anashikilia(five W and H); Lini, nani, wapi, kipi, kwa namna gani na kwanini.

### TAALUMA VS MUUNGANO

Hivyo, tafsiri hiyo pana ya misingi kitaaluma, nayo ina sura yake ndani ya historia ya Muungano. Nayo ina msingi yake, ambayo leo Rais Dk. Samia Suluhu Hassan na Dk. Hussein Mwinyi wa Zanzibar wanaidumisha ikiwa na vipengele vikuu vinne, kama taaluma basi ndio; anatomy and physiology, '5R' au KKK ya muungano.

Kwanza, walioshi zana za Tanganyika na Zanzibar kihistoria walidumu kindugu na kuchagamana kimaisha, hata kabla ya muungano wa sasa, ukiimarishwa zaidi na uswahiba wa Mwalimu Julius Nyerere na Mzee Abeid Aman Karume, wakipeana mbinu za kisiasa kumng'oa mkoloni.

Watu hao walishirikiana moja kwa moja, wakisafiri wote kwenda ughaibuni kwa watawala kudai haki yao ya uhuru, huku raia wao wakaingiliana katika makazi na maisha ya kawaida pande mbili.

Eneo la pili likagusa na tukio la mwaka 1964, kuchanganya udongo wa pande mbili. Kisheria jina la Tanganyika lilikufa na kuzaliwa Tanzania.

Ni zama hizo kukashuhudiwa mengi ya kimuungano sasa Tanzania Bara na Zanzibar, mathalan kukawapo vikosi vya ulinzi na usalama vya pamoja, bunge na miaka mwili baadae, rasmi ikaanza kutumika nchini Benki Kuu ya Tanzania (BOT) mwaka 1966.

Ni katika mwaka huo wa 1964, Tanzania ikapata zawadi ya Muungano, alipoteuliwa kijana mwenye miaka 24 Balozi Salim Ahmed Salim, Rais Karume Makamu wa Rais, akimpendekeza kwa swahiba wake Rais Nyerere, kupata, kwenda kuwakilisha taifa nchini Misri.

Katika mizunguko yake ya ubalozi akaonyesha makubwa, hata akaipa sifa Tanzania alipotikisa dunia akiwania kuwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, hata alipoachwa kwa 'mizengwe ya kura za veto; bado Waafrika wenzake wakamchagua kuwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika (OAU), akitumika kwa vipindi vitatu.

Haikushangaza kijana huyo wa Unguja, baadaye jina lake liling'ara mwaka 1985 katika mbio za kusaka mrithi wa Mwalimu Nyerere, alipoamua kung'atuka. Bado katika damu ya Muungano, kura zilirejea Zanzibar, kwa Mzee Ali Hassan Mwinyi, akaongoza nchi kwa awamu mbili.

Mfumo huria wa kiuchumi na kisiasa, mwaka 1992, uliridhiwa chini ya uongozi wake na hata uchaguzi mkuu wa vyama vingi, ukafanyika akikabidhi nchi kuacha kijiti kwa Mtanzania mwingine wa awamu ya tatu, ikamuangukia Benjamin Mkapa.

Kwa lingine ni kwao Nyerere na Karume wakichangamana kwa mengi ya Muungano, kuliko zama zile za kusaka uhuru, mwaka 1977 vyama vya TANU na ASP, vilivyoshiriki kuanzisha uhuru wa nchi, vikaungana na kuzaliwa Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Ilikuwa ni hatua kubwa ambayo ikawaundia Watanzania sura na undugu, kukishuhudiwa Wanzazibari ambao kwao hapakuwapo baadhi ya huduma muhimu za maendeleo yao kama vyuo vikuu na hospitali kubwa huko nyuma, wakavuka mpaka kuja kupata maslahi yao tiba na hata kitaaluma kwa umoja mkubwa.

Hapo ndipo inatia hamasa kwamba, Rais wa sasa Dk. Samia Suluhu Hassan ni mhitimu wa Chuo cha Maendeleo Mzumbe (IDM), ambayo sasa chuo kikuu, katikati ya miaka ya 1980.

Vivyo hivyo, katiba ya nchi yenye maslahi ya pamoja na ikitumikia wafanyabiashara wanavuka mipaka na mengine mengi, utamaduni wa hadi siku ukingiliana, kama ilivyo shughuli za kupata maslahi hata kijamii kama vile ndoa.

Katika mifumo ya uongozi wa nchi, kuchangamana leo kunabeba sura ya ukomavu, inayoleta tabasamu. Rais Dk. Samia, mzaliwa wa Unguja anaongoza gurudumu la Muungano.

Huko Zanzibar, Dk. Mwinyi ambaye hata wakati fulani alishakuwa mbunge wa Mkuranga na kisha ndani ya Unguja, anaongoza Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ).

Katika staili inayotumika hadi sasa kati ya marais hao, Dk. Samia na mtaalamu tiba, Dk. Mwinyi ili kuenzi sura njema ya muungano iliyoasisiwa zama hizo na ndio maana hadi sasa, kunaendelea mijadala na uwajibikaji wa kinachoitwa "Kamati ya Kero za Muungano' kuifaidisha yaliyo mema na kuondoa kasoro katika kufuta ya kasoro zinazojitokeza.

Mfano hivi sasa, inashuhudiwa namna Rais Dk. Mwinyi akitanua Uchumi wa Buluu visiwani kwa mafanikio makubwa, nadharia aliyoiuza kwa majirani wa Muungano, sasa ikitumika kunufaisha walio Tanzania bara, ikishuhudiwa katika maeneo kama ya Pwani ya Kilwa, imegeuka kuwa nguzo ya uchumi kwa kinamama hao, kama ilivyo Zanzibar.

Sasa, takwimu zinaonyesha robo tatu ya Watazania wamezaliwa baada ya Muungano, kwamba wameukuta maishani, mmojawapo akiwa Rais Dk. Mwinyi aliyeiona dunia muda mfupi baadaye, huku Rais Dk. Samia, Muungano ulimkuta katika umri wa 'kidali poo'.

Hapo napo unaonyesha tena Muungano huo wa kiutawala, Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano, Dk. Samia na Dk. Mwinyi, Rais wa Awamu ya Nane Zanzibar wakiunda mvuto wa aina yake, juzi 'akichombeza' kuboresha Muungano kwa kurejesha Kombe la Soka la Muungano, lililoachwa kwa muda.

MIAKA 60 YA MUUNGANO

# Mwinyi atambua mchango wa wanawake katika Muungano



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi

**Na Romana Mallya**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema wanawake walikuwa na mchango mkubwa katika kufanikisha kufanyika kwa Muungano ambao unatimiza miaka 60 ya kuasisiwa kwake kwa mafanikio makubwa.

Dk. Mwinyi alisema hayo juzi jijini Dar es Salaam wakati wa mdahalo wa nafasi ya mwanamke katika kipindi cha miaka 60 ya Muungano wa Tanzania ulioandaliwa na Jumuiya ya Umoja wa Wanawake wa Tanzania (UWT).

"Ninaomba niwataje wachache kati ya wengi walioshiriki harakati za ukombozi wakiwamo Bibi Titi Mohamed, Liti Kidanka, Mwami Thelesa, Mwana Makuka, Siti binti Saad, Fatma Amour, Lucy Lameck, Mtumwa Kitete, Tatu Mzee, Khadija Jabiri, Maryam Mohamed, Tumwa Fikirini, Salama Mzee, Safia Kawawa, Mama Maria Nyerere, Mama Fatma Karume na wengineo," aliwataja

Dk. Mwinyi alisema wazee hao ni mfano mzuri wa wanawake waliojitoa na kushirikiana na waasisi wa taifa katika kuwaletea uhuru watanzania na Muungano wa nchi.

Alisema hawawezi kusahau mchango wao katika maendeleo ya nchi hivi sasa ndani ya miaka 60 ya Muungano.

"Hawa na wanawake wengine wengi walishika nafasi mbali mbali za uongozi katika nchi yetu na vyama vyetu vya siasa na Jumuiya zake wanabaki kuwa ni vigezo vizuri vya utendaji na ushiriki wa wanawake katika kuleta maendeleo ya Watanzania.

"Bila ya shaka utendaji na mchango wa viongozi hawa umefanya wanawake wenzao kuendelea kuaminika katika nafasi mbalimbali za uongozi kama anavyodhihirisha hilo Rais Samia Suluhu Hassan," alisema.

Dk. Mwinyi alisema wanaridhika na utendaji kazi wa Rais Samia ambao umeipatia sifa nchi na kuwawezesha kupiga hatua kubwa za maendeleo katika sekta zote katika kipindi kifupi cha uongozi wake.

Alisema muungano wa Tanzania ambao unatimiza miaka 60 ya kuasisiwa kwake, umeiletea sifa za pekee na heshima nchi, faida nyingi za kikuchumi, kisiasa na kijamii kwa wananchi wa pande zote mbili za Muungano. "Dhamira njema ya waasisi wa taifa letu ya kuunganisha nchi zetu mbili imeendelezwa na viongozi wa pande zote mbili za Muungano kwa kuudumisha, na kuimarisha kwa kuzipatia ufumbuzi changamoto zilizojitokeza hadi sasa na hivyo kuufanya uwe imara zaidi," alisema.

Kuhusu uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu, Dk. Mwinyi, alisema ni wajibu wao kufanya maandalizi ya kutosha katika ushiriki wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika chaguzi zote na kuhakikishia CCM inapata ushindi mkubwa.

"Tuendelee kukiimarisha chama chetu na jumuiya zake kwa kuongeza idadi ya wanachama na kuhakikisha wanachama wetu wote na wapenzi wa CCM wanajiandikisha katika Daftari la Wapiga Kura la NEC na ZEC," alisema.

Dk. Mwinyi alitoa hamasa kwa wanawake kushiriki kwa wingi kugombea nafasi wakati wa uchagizi utakapofika, kwa kuwa wapo wengi wenye uwezo mkubwa wa uongozi.

"Ninatoa pongezi kwa kazi kubwa inayofanywa na wanawake hasa kupitia UWT katika kuwaletea maendeleo Watanzania na kukiimarisha Chama Cha Mapinduzi. Natoa shukrani zangu tena kwa uongozi wa UWT kwa kuandaa Mdahalo huu katika Maadhimisho ya Miaka 60 ya Muungano na kunialika kuwa mgeni rasmi," alisema Dk. Mwinyi.







# Butiku: Tuulinde utanzania kwenye Muungano

**Na Sabato Kasika**

MWENYEKITI wa Taasisi ya Mwalimu Nyerere Foundation, Joseph Butiku (pichani) amesema, Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ni wa wananchi wa pande mbili, na kutaka watukuze utanzania zaidi ili kuendelea kuimarisha muungano huo.

Butiku alisema hayo katika kongamano la miaka 60 ya muungano wa Tanganyika na Zanzibar lililoandaliwa na Chuo cha Ustawi wa Jamii jijini Dar es Salaam jana.

Alisema baada ya Muungano wa mwaka 1964, nchi imekuwa moja yenye serikali mbili, na kwamba ni vyema kikifanya kizazi cha sasa kutambua maana ya muungano huo na kuusemea vizuri.

"Muungano si wa Nyerere wala Karume au CCM (Chama Cha Mapinduzi), viongozi hao walionyesha njia wananchi wakakubali. walioukubali walikuwa na uwezo wa kukataa, hivyo ni vyema utukuzwe na pia maoni yao yaheshimiwe," alisema Butiku.

Mwenyekiti huyo alifafanua kuwa Muungano huo ni wa hiyari, na kwamba umesaidia kuwafanya wananchi kuendelea kushirikiana kwa karibu kwa kila nyanja.

"Lakini pamoja na hayo zipo baadhi ya kero za muungano ambazo zimekuwa zikilalamikiwa na wananchi, kwa kuwa wao ndio wenye muungano, muwasikilize na kuzitafuatia ufumbuzi," alisema.

Akizungumza wakati wa uwasilishaji wa mada ya isemayo elimu juu ya muungano tulikotoka tulipo', Dk. Cast Rengua kutoka chuo hicho, alisema, wakati Tanganyika na Zanzibar zinaungana, kulikuwa na chuo kimoja na kwamba sasa vipo 49 vya serikali vikiwa 19 na binafsi 30.

"Vilevile, wakati huo kulikuwa na wataalam wachache, lakini sasa kila mwaka vyuo vinazalisha wataalam 10,000. Hii inaonyesha tunazidi kupiga hatua kwenda mbele tunapotimiza miaka 60 ya muungano," alisema Dk.Cast.

Akizungumzia mada ya 'amani, mshikamano ndio nguzo ya maendeleo ya taifa letu', Dk. Peter Mgawe kutoka chuo hicho, alisema, hivyo vyote vimedumu kwa miaka 60 kutokana na uhusiano wa karibu kati wananchi wa pande hizo mbili.

"Lakini pia Kiswahili kimesaidia kuimarisha muungano ambao sasa imetimiza miaka 60 tangu uanzishwe," alisema Dk. Mgawe.

Mhadhiri wa Chuo cha Diplomasia, Abbas Mwalimu, alisema jiografia ndio ilisababisha wazungu wawagawanye Watanganyika na Wazanzibar.

"Viongozi wetu, Mwalimu Nyerere na Karume wakaamua kuunganisha jamii yetu ambayo iligawanywa kwa sababu za kijiografia na sasa Muungano wetu unaendelea," alisema Mwalimu.









## Mpango ataka taasisi kujenga ofisi binafsi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MAKAMU wa Rais Dk. Philip Mpango, amezitaka taasisi zote za serikali ambazo zimehamia Dodoma, kuanza mchakato wa ujenzi wa majengo binafsi ili kuondokana na gharama za kulipa kodi ya pango.

Dk. Mpango aliyasema hayo jana jijini hapa baada ya kuzindua jengo la ofisi za makao makuu ya Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF).

Alisema taasisi ambazo tayari zipo Dodoma zinapaswa kuwa na ofisi binafsi ili kuondokana na gharama kubwa za kodi ya pango kwenye majengo ya watu na taasisi binafsi. "Taasisi zote zinapaswa kuwa na majengo ya ofisi zake binafsi ili kuondokana na adha ya kukodi na kulipa fedha nyingi kwa ajili ya pango la ofisi. Pia taasisi zote zinapaswa kuhakikisha zinatekeleza agizo la serikali la kuhamia Dodoma.

"Wale ambao bado hawataki kuhama wanaendelea kubaki kule waliko, sisi tutawahamisha kwa njia yetu kwani lazima kila taasisi ya serikali kutekeleza agizo la serikali kuhamia makao makuu ya nchi" alisema.

Dk. Mpango pia alisema pamoja na kazi nzuri inayofanywa na UCSAF, bado kuna haja kwa mfuko huo kuhakikisha unaendelea kusimamia ujenzi wa minara kwa kushirikiana na sekta binafsi ili kufikisha huduma za mawasailiano vijijini.

"Taifa letu limepiga sana hatua katika sekta mbalimbali ikiwamo hii ya TEHAMA (Teknolojia ya Habari na Mawasiliano) kwa kipindi hichi cha miaka 60 ya Muungano kwani wakati Muungano unaanzishwa mwaka 1964, serikali ilikuwa na kompyuta moja tu lakini hivi sasa matumizi ya kompyuta na intaneti yameongezeka sana,"alisema.

Waziri wa Habari, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano Nape, Nnauye, alisema mafanikio ya wizara hiyo yanatokana na utashi wa kisiasa alio nao Rais Samia Suluhu Hassan.

Alisema kutokana na uwekezaji katika sekta ya TEHAMA nchini hakuna Mtanzania ambaye ataachwa nyuma bila kuunganishwa na mifumo ya mawasiliano. Pia alisema UCSAF imewezesha watanzania wengi waishio vijijini na maeneo yasiyo na mvuto kibiashara kwa watoa huduma kuweza kuunganishwa na huduma za mawasiliano kupitia ruzuku inayotolewa na mfuko huo kwa ajili ya ujenzi wa minara ya mawasiliano yenye teknolojia kuanzia 2G hadi 5G.

Aliwahakikishia Watanzania kuwa hakuna atakayeachwa bila kuunganishwa na huduma za mawasiliano na kwamba mradi wa ujenzi wa minara 758 unaoendelea kutekelezwa na UCSAF kwa kushirikiana na watoa huduma, utawaunganisha watu milioni nane kwa wakati mmoja.





# Matukio ya udhalilishaji kijinsia Zanzibar yapungua

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MATUKIO ya udhalilishaji wa kijinsia visiwani Zanzibar kwa Machi mwaka huu yamepungua kutoka 175 kipindi cha Februari hadi 125 mwezi huu.

Akiwasilisha matukio ya udhalilishaji kwa kipindi cha Machi kwa waandishi wa habari, Mkuu wa Divisheni ya Takwimu za Jinsia na Ajira kutoka Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Ramla Hassan Pandu alisema waathirika wengi walikuwa watoto sawa na asilimia 81.6, wanawake asilimia 13.6 na wanaume asilimia 4.8.

Ramla alisema katika matukio hayo ubakaji unaongoza ambao ulikuwa na matukio 67, shambulio 29, ulawiti nane, kuingilia kinyume na maumbile sita, kutorosha manne na kukashifu 11.

Alisema Wilaya ya Magharib A Unguja, imeripotiwa kuwa na matukio mengi ukilinganisha na wilaya nyingine ambayo ilikuwa na matukio 38 ikifuatiwa na Wilaya ya Magharib B ilikuwa na matukio 34.

"Wilaya ya Kusini imeripotiwa kuwa na idadi ndogo ya matukio, tukio moja sawa na asilimia 0.8 ikilinganisha na wilaya zingine ambapo Wilaya ya Micheweni hakukuripotiwa tukio lolote kwa kipindi cha Machi 2024," alisema.

Kwa upande wa matukio ya ubakaji, alisema Wilaya ya Magharibi B Unguja, kulikuwa na idadi kubwa ya matukio ya kubaka yapatayo 20 ikilinganishwa na wilaya nyingine.

Hata hivyo alisema kati ya matukio 67 ya ubakaji yaliyoripotiwa kwa kipindi cha Machi mwaka huu ni saba ya ubakaji yameripotiwa kwa wanawake na matukio 60 yameripotiwa kwa wasichana.

Alisema jumla ya wafungwa wa makosa ya udhalilishaji waliopelekwa gerezani kutoka Januari hadi Machi mwaka huu ni 35 na mahabusu 143, wengi wao wakiwa kati ya umri wa miaka 18 hadi 29.

# Serikali, NMB kuboresha mifumo ukusanyaji mapato

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

WAKATI wajumbe wa Mkutano Mkuu wa 38 wa Mwaka wa Jumuiya ya Tawala za Mitaa (ALAT Taifa), wakipewa angalizo kuwa bila mapato na makusanyo hakuna serikali imara, Mdhamini Mkuu wa mkutano huo, Benki ya NMB imeahidi kuendeleza maboresho ya kimkakati ya mifumo ya ukusanyaji mapato.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mohammed Mchengerwa, aliyasema hayo juzi wakati akifungua mkutano huo unaokutanisha pamoja wajumbe zaidi ya 600, wakiwamo mameya wa majiji na manispaa, wenyeviti na wakurugenzi wa halmashauri 184 (za Tanzania Bara).

Waziri Mchengerwa alikuwa anamwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan katika ufunguzi wa mkutano huo wa siku tatu, unaofanyika chini ya kaulimbiu ya 'Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ni Jambo Letu; Shiriki kwa Maendeleo ya Taifa,' akitoa maelekezo na miongozo ya kisera kwa watendaji hao wa Mamlaka za Serikali za Mitaa. "Rais amenituma kuwaeleza namna alivyotamani sana kuwa nanyi katika mkutano huu, hasa kutokana na umuhimu wenu kwa Serikali na Wananchi, anatambua na kuthamini majukumu ya ALAT kwa maendeleo ya taifa, ndio maana amesisitiza endeleeni kutanua vyanzo vya mapato na makusanyo, na kusimamia miradi ya maendeleo.

"Bila mapato, hakuna serikali imara ndio maana amewataka kuwa wabunifu wa vyanzo vipya vya mapato katika halmashauri na majiji, kupambana na mashine hewa, zinazozimwa wakati wa makusanyo na kuisababishia serikali hasara. Nendeni mkasimamie mianya ya upotevu na kuzuia matumizi yasiyo ya lazima," alisema. Awali, NMB kupitia Ofisa Mtendaji Mkuu wake, Ruth Zaipuna, iliahidi kuendelea kuboresha sekta za kimkakati ikiwamo mifumo ya ukusanyaji mapato, huku ikitangaza kutenga Sh. bilioni nane za Programu ya Uwekezaji kwa Jamii (CSI), zikiwamo Sh. bilioni 2.5 za ujenzi wa shule maalum jijini Dodoma.

Akizungumza katika mkutano huo ambao umedhaminiwa na benki yake kwa Sh. milioni 120, Bi. Zaipuna alisema NMB inajivunia Makusanyo ya Mapato ya Serikali ya zaidi ya Sh. Trilioni 9.8 tangu mwaka 2018, na kuwa siri ya mafanikio hayo ni ushirikiano wao na halmashauri zote 195 (184 za Tanzania Bara na 11 za Tanzania Zanzibar).

"NMB imeendelea kushirikiana vyema na Serikali zote mbili katika kuboresha mifumo ya ukusanyaji mapato, ambako tumewekeza katika teknolojia na mifumo bora na rahisi ya kusaidia serikali kukusanya mapato na kuwezesha kukusanya zaidi ya Sh. trilioni 9.8 tangu mwaka 2018.

"Kupitia Programu ya Uwekezaji kwa Jamii (CSI), NMB tumetenga kiasi cha Sh. bilioni nane. Kati yake, Sh. bilioni 2.5 tutazitumia kujenga shule maalum jijini Dodoma na Sh. bilioni 5.4 za kusaidia utatuzi wa changamoto katika sekta za elimu, afya, majanga na utunzaji mazingira," alisema Zaipuna.

Alibainisha kwamba kwa miaka miwili ya 2022 na 2023, NMB kupitia CSI, imetumia zaidi ya Sh. bilioni saba, na kwamba kutokana na faida baada ya kodi ya Sh. bilioni 542 iliyopata mwaka jana, ilistahili kutenga Sh. bilioni 5.4 za CSI mwaka huu, lakini kiasi kimeongezeka hadi bilioni nane ili kufanikisha ujenzi wa shule mkoani Dodoma.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mohamed Mchengerwa (wa pili kushoto) akikabidhi cheti cha shukrani kwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna wakati wa Mkutano Mkuu wa 38 wa Jumuiya ya Tawala za Mitaa Tanzania (ALAT), jijini Zanzibar. Kushoto ni Makamu Mwenyekiti wa ALAT, Sima Constantine Sima na (kulia) ni Ofisa Mkuu wa wateja wakubwa wa Serikali wa benki hiyo, Alfred Shao. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yawahakikishia ushirikiano mashirika ya kimataifa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema Zanzibar ipo tayari kushirikiana na wadau na mashirika ya kimataifa ili kusaidia upatikanaji wa huduma bora zaidi za afya kwa wananchi na jamii kwa jumla.

Aliyasema hayo jana ofisini kwake Migombani Mjini Zanzibar alipokutana na ujumbe wa Shirika la Kimataifa la CBM, linalojishughulisha na utoaji wa huduma za afya kwa jamii katika kukabiliana na changamoto za kiafya.

Alisema hatua hiyo inatokana na ukweli kwamba licha ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutoa kipaumbele katika sekta ya afya ili kuwasaidia wananchi lakini bado kuna changamoto nyingi za kiafya katika jamii zinazoendelea kujitokeza ambazo zinahitaji juhudi za wadau katika kukabiliana nazo.

Alisema kwamba pamoja na juhudi za serikali kufanya hivyo lakini mahitaji ya huduma bora za kiafaya katika maeneo mbalimbali bado ni makubwa na yanahitaji juhudi za wadau kusaidia upatikanaji wa huduma hizo.

Hivyo, aliutaka ujumbe wa shirika hilo linalojishughulisha na utoaji wa huduma za kiafya katika nchi mbalimbali duniani ikiwemo kusaidia watu wenye ulemavu, matatizo ya macho na mengineyo kufikiria kupanua wigo zaidi wa huduma zao Zanzibar.

Alisema yapo maeneo mengi yanayohitaji misaada na mashirikiano ya wadau hasa katika kuwajengea uwezo wataalumu wa ndani pamoja na upatikanaji wa nyenzo za kiafya kwa jamii ili kustawisha upatikanaji wa huduma bora zinazohitajika kwa jamii.

Aidha, alilitaka shirika hilo kuangalia uwezekano wa kusaidia eneo la elimu ya afya na kinga katika kuzikabili changamoto za maradhi yanayowakabili wananchi wa Zanzibar.

Akizungumzia suala la huduma kwa watu wenye ulemavu, Othman alisema kwamba serikali imefanya mageuzi makubwa ya kisera na kisheria, ili kurahisisha upatikanaji wa huduma bora kwa watu wenye ulemavu lakini jitiada izo zinahitaji ushirikiano wa wadau ili kutimiza malengo yaliyowekwa.

Naye Mkurugenzi Mkazi wa Shirika hilo nchini, Nesia Mahenge , alisema Zanzibar walianza na mradi wa ushirikiano na Wizara ya Afya uliojikita utoaji wa huduma, kuwajengea uwezo wataalamu wa ndani ikiwa ni pamoja na kuhakikisha huduma bora kwa watu wenye ulemavu tangu mwaka 2022.

Hata hivyo, alisema licha ya mradi huo kutekelezwa katika Kisiwa cha Unguja pekee lakini wamebaini pia kuwepo mahitaji makubwa ya huduma kama hizo kutolewa katika Kisiwa cha Pemba.

Kadhalika, aliishukuru Serikali ya Zanzibar kwa ushirikiano mkubwa waliopata katika utekelezaji wa mradi huo ikiwa ni pamoja na kupata fursa ya kukutana na viongozi wakuu wa nchi kubadilishana mawazo na kupata ushauri kuhusu huduma za mradi huo. Shirika hilo linalojikita katika kusaidia utoaji wa huduma za afya kwa watu wenye ulemavu linafanya kazi katika nchi zaidi ya 30 duniani, limekuwa likitoa ufadhili wa masomo kwa wataalamu wa kada za afya ili kuwajengea uwezo.

# EWURA yasajili kampuni 2,029 sekta ya mafuta, gesi asilia

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imesajili kampuni za wazawa 2,029 na wataalamu 198 kwenye kanzidata, ikiwa ni utekelezaji wa mikakati ya serikali ya kuwashirikisha Watanzania katika sekta ya mafuta na gesi asilia.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko aliyasema juzi bungeni alipokuwa akiwasilisha utekelezaji wa bajeti ya wizara hiyo kwa mwaka 2023/24 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2024/25.

Alisema kampuni 157 zimesajiliwa na zinapata fursa za kuuza bidhaa na kutoa huduma mbalimbali kwenye miradi inayoendelea na wataalamu 187 wa ndani wenye ujuzi mbalimbali katika tasnia ya mafuta na gesi asilia wamesajiliwa katika mfumo na kanzidata za shughuli za petroli.

Aidha, alisema takribani kampuni 250 zilipata zabuni za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja katika mradi EACOP na miradi mingine katika sekta ndogo ya gesi asilia.

Kuhusu usimamizi na udhibiti wa shughuli za mkondo wa kati na chini wa gesi asilia, Dk.Biteko alisema serikali kupitia EWURA iliendelea kusimamia shughuli za gesi asilia kwa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara katika miundombinu ya uchakataji, usafirishaji na usambazaji wa gesi asilia na vituo vya kujazia gesi kwenye magari (CNG) katika mikoa ya Mtwara, Lindi, Pwani na Dar es Salaam.

Alifafanua kuwa ukaguzi huo maalum ulishirikisha EWURA, Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB) ili kuhakikisha usalama kwenye eneo la utaalam, vifaa na mazingira ya utekelezaji wa shughuli zinazohusu matumizi ya gesi asilia kwenye magari.

Kadhalika, alisema hadi kufikia Machi 2024, EWURA ilitoa vibali sita kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kusambaza gesi asilia viwandani na vituo vya CNG.



Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, January Makamba (kulia) akiwa na Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), Dk. John Mduma, wakati akizungumza na mabalozi wanaoiwakilisha Tanzania nje ya nchi, kwenye Shule ya Uongozi ya Julius Nyerere, Kibaha mkoani Pwani mapema wiki hii. WCF hutumia ofisi za Balozi za Tanzania nje ya nchi ili kuthibitisha uhalali wa madai ya mfanyakazi, anayeumia, kuugua au kufariki dunia wakati akitekeleza majukumu ya mwajiri nje ya mipaka ya nchi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## RC ashtukia ufisadi ujenzi Sekondari ya Kitaraka

**Na Thobias Mwanakatwe,** ITIGI

MKUU wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, ameshtukia upigaji wa fedha katika ujenzi wa Shule ya Sekondari Kitaraka iliyopo Halmashauri ya Itigi wilayani Manyoni ambayo serikali ilitoa Sh. milioni 470 kujenga.

Kufuatia hali hiyo, amemwagiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Itigi, Ayoub Kambi kumpeleka mkaguzi kwenda kukagua jinsi fedha hizo zilivyotumika kwani kiasi cha fedha kilichobaki Sh. milioni 1.8 hakiwezi kutosheleza kumalizia ujenzi uliobaki.

Awali Mkuu wa Shule ya Sekondari Kitaraka, Aman Mwamakula, alisema serikali ilitoa Sh.milioni 470 kujenga shule hiyo katika mwaka wa fedha wa 2021/2022 kupitia Mradi wa Uboreshaji wa Elimu ya Sekondari Tanzania (SEQUIP).

Alisema mradi wa ujenzi wa shule hiyo ambao ulianza Aprili 2022 ulisimamiwa na kamati za utekelezaji na ujenzi kuanzia ngazi ya halmashauri zinazohusisha wataalam wa halmashuri kwa mfumo wa manunuzi ujulikanao 'Force Account' (akaunti ya dharura).

Mwamakula alisema mradi huo ulihusisha ujenzi wa jengo la utawala, madarasa nane, ofisi nne, maabara ya kompyuta, maktaba, maabara tatu za sayansi, matundu ya vyoo vya wanafunzi na tangi la maji na nguzo.

Alisema hadi sasa majengo yaliyokamilika ni jengo la utawala, madarasa sita, ofisi tatu, vyoo vya wanafunzi na walimu na tangi la maji na nguzo ambapo kiasi cha fedha kilichobaki ni Sh. milioni 1.8.

Mwamakula alisema majengo ambayo bado ujenzi wake haujakamilika kwenye umaliziaji ni maabara tatu, maktaba, madarasa mawili na jengo la ICT.

# Watatu kortini kukutwa na kilo 424 dawa za kulevya

**Na Gwamaka Alipipi**

WATUHUMIWA watatu wamefikishwa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kibaha mkoani Pwani, wakikabiliwa na mashtaka ya kusafirisha dawa za kulevya aina ya methemphetamine kilogramu 424.84 na heroin hydrochloride gramu 158.24.

Watuhumiwa hao ni Rajabu Kisambwanda (42) mkazi wa Kerege Matumbi, Bakari Said (39) mkazi wa Kunduchi Mtongani na Hillary Rhite (35) mkazi wa Kunduchi Sodike.

Akisoma hati ya mashtaka Wakili wa Serikali, Agness Ndanzi mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Joyce Mkhoi alidai kuwa washtakiwa hao walikutwa wakisafirisha dawa hizo za kulevya Aprili 10, 2024 eneo la Zinga Wilaya ya Bagamoyo mkoani Pwani.

Wakili Ndazi aliendelea kuieleza mahakama kuwa, katika tukio lingine, tarehe hiyohiyo mshtakiwa Said mkazi wa Kunduchi Mtongani alikutwa akisafirisha dawa za kulevya aina ya heroin hydrochloride yenye uzito wa gramu 158.24.

Hata hivyo, washtakiwa wote watatu hawakuruhusiwa kujibu chochote kwani mahakama hiyo haina mamlaka ya kisheria kusikiliza shauri hilo na watafikishwa tena mahakamani hapo Mei 7, 2024 kwa ajili ya kutajwa.

Watuhumiwa waliofikishwa mahakamani ni kati ya watuhumiwa 21 waliotangazwa na Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) Aprili 22, 2024.

# Israel yabanwa kuhusu makaburi ya halaiki Gaza

**LONDON,** Uingereza

NCHI mbalimbali duniani ikiwamo Umoja wa Ulaya zimeunga mkono wito wa Umoja wa Mataifa wa kutaka kufanyike uchunguzi huru kuhusu kugundulika kwa makaburi ya halaiki kwenye hospitali mbili katika Ukanda wa Gaza.

Msemaji wa Umoja wa Ulaya, Peter Stano, alisema kuwa tukio hilo linalazimisha kufanyike kwa uchunguzi huru ili kubaini ukweli kuhusu tuhuma na mazingira yote yanayoendana na ripoti hiyo.

"Hili ni jambo linatulazimisha kutoa wito wa kufanyika kwa uchunguzi huru kuhusu tuhuma na mazingira yote, kwa sababu inajenga hisia kwamba kunaweza kuwa na ukiukwaji wa haki za binadamu za kimataifa," alisema Stano.

**Hili ni jambo linatulazimisha kutoa wito wa kufanyika kwa uchunguzi huru kuhusu tuhuma na mazingira yote, kwa sababu inajenga hisia kwamba kunaweza kuwa na ukiukwaji wa haki za binadamu za kimataifa.**

Aliongeza "Ndiyo maana ni muhimu kuwa na uchunguzi huru na kuhakikisha uwajibikaji."

Hivi karibuni Umoja wa Mataifa ulitoa wito kufanyika uchunguzi wa kimataifa na kushirikishwa katika kujua ukweli wa kupatikana kwa miili hiyo.

Pia iliongeza kuwa imehuzunishwa na uharibifu uliofanyika dhidi ya hospitali mbili kubwa ndani ya Ukanda wa Gaza, za Al-Shifa na Nasser Medical Complex.

Shirika la Ulinzi wa Raia la Gaza lilisema kwamba wafanyakazi wa afya waligundua karibu miili 340 ya watu wanaodaiwa kuuawa na kuzikwa na vikosi vya Israel ndani ya kaburi moja kwenye uwanja wa hospitali ya Nasser.

Hata hivyo, jeshi la Israel (IDF) lilijibu ripoti hiyo kuwa haina msingi na kwamba wanajeshi wake walifanyia uchunguzi miili ya watu iliyozikwa na Hamas kwa ajili ya kutafuta raia wao waliotekwa nyara.

Wakati huo huo, polisi nchini Marekani wamewakamata watu 93 katika Chuo Kikuu cha kusini mwa California (USC) katika jimbo la Los Angeles katika kukabiliana na maandamano ya wanafunzi wanaopinga vita vinavyoendelea Ukanda wa Gaza.

Polisi wakiwa na vifaa vya kutuliza ghasia walisambaratisha kambi ya watu wanaounga mkono Palestina ndani ya chuo hicho, na kutoa amri ya watu kutokusanyika.

Wakati watu hao wanatiwa mbaroni, maandamano mengine yaliripotiwa kufanyika katika Chuo Kikuu cha Texas.

Vyuo vikuu vingi nchini Marekani vimegubikwa na ongezeko la ghasia za wanafunzi na wengine wakijaribu kukusanyika kupinga operesheni ya kijeshi inayofanywa na Israel katika Ukanda wa Gaza.

Mamia ya waandamanaji wamekamatwa kwenye vyuo kadhaa nchini humo vikiwamo Columbia, Yale na Chuo Kikuu cha New York.

Vita vya Gaza vilianza Oktoba 7, mwaka juzi baada ya watu wenye silaha wakiongozwa na Hamas kufanya shambulio ambalo halijawahi kushuhudiwa kusini mwa Israel tarehe 7 Oktoba, na kuua watu 1,200, na kuwashikilia mateka 253. **BBC**



Raia wa jiji la Nairobi akikabiliana na mafuriko baada ya mvua nyingi kunyesha nchini Kenya katika siku za hivi karibuni. **PICHA: EPA**

# Apple yadaiwa kutumia madini haramu

**PARIS,** Ufaransa

SERIKALI ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) imeishutumu kampuni ya teknolojia ya mawasiliano ya Apple kwa kutumia madini yaliyochimbwa kinyume cha sheria kutoka eneo lake la mashariki kwa kuunda bidhaa zake.

Shirika la habari la AFP limeripoti kuwa mawakili wenye makazi yao nchini Ufaransa, waliitumia kampuni hiyo ombi rasmi ya kuitaka isitishe mara moja biashara hiyo.

Mawakili hao walisema kununua madini hayo kwa ajili ya kutengeneza bidhaa zake ni kinyume na huenda ikachukuliwa hatua za kisheria iwapo itaendelea kufanya hivyo.

Aidha, jopo hilo la mawakili liliishtumu kampuni ya Apple kwa madai ya kununua madini yaliyoingizwa nchini Rwanda kutoka DRC kinyume cha sheria kabla ya kusafishwa na kuingizwa katika soko la kimataifa.

Wakionyesha ripoti ya mwaka 2023, kuhusu madai ya matumizi ya madini ya migogoro ambayo kampuni hiyo inatumia kutengeneza bidhaa za gharama kubwa.

Hata hivyo, kampuni ya Apple, iliambia AFP kwamba haijapata sababu zozote za kimsingi ambayo inahitimisha kuwa madini yoyote yanayodaiwa kutumika kwa bidhaa zake kufikia tarehe 31 mwezi Desemba mwaka 2023 yalitokana na njia yoyote ile kufadhili au kunufaisha makundi yenye silaha nchini DRC. **DW**

## Mafuriko yasaidia wafungwa kutoroka gerezani

**ABUJA,** Nigeria

ZAIDI ya wafungwa 100 wametoroka baada ya gereza moja nchini Nigeria kukumbwa na mafuriko ya maji yaliyotokana na mvua kubwa kunyesha.

Kwa mujibu wa mamlaka nchini humo, wafungwa 118 walifanikiwa kutoroka katika Gereza la Suleja, lililoko karibu na mji mji mkuu wa Abuja, lakini 10 walikamatwa.

Polisi nchini humo wametangaza msako mkali kuwatafuta wengine ambao hadi sasa hawajakamatwa.

Hata hivyo, utambulisho wa wafungwa hao bado haujabainika, lakini kuna hofu kuwa baadhi yao wanaweza kuwa wahalifu hatari.

Hata hivyo taarifa kutoka katika gereza hilo ilisema wanafanya kazi na vyombo vingine vya usalama na kuwatuliza watu kuendelea na shughuli zao za kawaida bila kuwa na hofu yoyote.

"Kwa kushirikiana na vyombo vingine vya usalama, kufikia sasa tumefanikiwa kuwakamata wafungwa 10 waliokuwa wakitoroka na kuwaweka chini ya ulinzi, huku tukiendeleza msako mkali wa kuwakamata wengine," ilisema taarifa kutoka idara ya magereza.

Taarifa hiyo iliongeza kuwa majengo mengi katika eneo la Suleja yalijengwa wakati wa ukoloni, hivyo yamezeeka. **BBC**

## Marekani, Niger kujadili kuwaondoa wanajeshi

**WASHINGTON,** Marekani

WIZARA ya Mambo ya Nje ya Marekani, imesema maofisa wake watakutana na wajumbe wa serikali ya Niger kujadili namna ya kuwaondoa wanajeshi wake nchini humo.

Utawala wa kijeshi wa Niger, umeiomba Marekani kuwaondoa wanajeshi wake waliomo nchini humo kutokana na kutoelewana kuhusu masuala kadhaa ambayo ni pamoja na kushindwa kutambua hatua zilizopigwa na taifa hilo kuelekea utawala wa kidemokrasia.

Kabla ya mapinduzi ya kijeshi ya mwaka jana, Niger ilikuwa mshirika mkubwa wa Marekani katika vita dhidi ya ugaidi na wanajeshi hao wamekuwa wakitoa mafunzo kwa vikosi vya nchi hiyo kwa ajili ya kupambana na makundi ya wanamgambo. **DW**

# FEI TOTO ATANGAZA RASMI 'VITA' KIATU CHA DHAHABU

Na Saada Akida

VITA ya kuwania ufungaji bora inaendelea kupamba moto baada ya kiungo mshambuliaji wa Azam FC, Feisal Salum 'Fei Toto', kusema ataendelea kupambana ili kuhakikisha anatumia nafasi vizuri kila nafasi kwa lengo la kufunga mabao katika michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo iko hatua ya lala salama.

Akizungumza na Nipashe jana, Fei Toto alisema malengo makubwa ya wachezaji wa Azam FC ni kufanya vizuri katika kila mechi na kwa upande wake suala la ufungaji bora itakuwa sehemu ya mipango aliyonayo kwa kujipanga kutopoteza nafasi.

**Fei Toto alisema anafurahi kuaminiwa na kupewa nafasi ya kucheza huku akiongeza ushirikiano mzuri kutoka kwa wachezaji wenzake utasaidia kufikia malengo yake.**

"Kikubwa ni kufuata maelekezo ya mwalimu pamoja na ushirikiano uliopo kutoka kwa wachezaji wenzangu, hakuna jambo ambalo litashindikana upande wao ikiwamo suala la kuvuna alama tatu katika kila mechi kwa sababu wanajipanga kutumia vizuri nafasi wanazotengeneza ili kufunga mabao mengi.

"Bado ninaimani kubwa ya kufanya vizuri kwa kufunga mabao kila ninapopata nafasi, pia ushirikiano mzuri ninaopata kutoka kwa wachezaji wenzangu ni hatua muhimu sana wetu kama timu," Fei Toto alisema.

Fei Toto amekuwa na msimu bora wa mwaka 2023/24 akiwa na uzi wa Azam, ameshafunga mabao 14, akiwa ndiye mchezaji namba moja kwa wazawa lakini anashika nafasi ya pili akiwa nyuma ya kinara, kiungo mshambuliaji wa Yanga, Stephane Aziz Ki.

Nyota huyo wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara amefunga mabao 15 katika michezo 23 waliocheza wakati Azam FC imeshuka dimbani mara 24.

Nafasi ya tatu katika orodha ya kupachika magoli inashikiliwa na mshambuliaji wa KMC FC, Waziri Junior ambaye ana mabao 11.




# *Wanariadha kibaruani Zanzibar*

Na Shufaa Lyimo

MASHINDANO ya riadha ya vijana wenye umri chini ya miaka 18 na 20 kwa nchi za Afrika Mashariki na Kati yanatarajiwa kuanza leo Zanzibar kwa kushirikisha wanariadha kutoka Bara na Visiwani.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa timu ya Tanzania Bara, Felix Chunga, alisema kikosi chake kina wanariadha 20 ambao walipatikana katika mashindano ya wazi yaliyofanyika mapema mwezi huu.

Chunga alisema wanariadha hao wamefanya maandalizi ya muda mrefu na wamekuwa na rekodi nzuri ya muda wanaotumia wakati wote wa mazoezi.

"Hawa ni wale wachezaji waliopatikana katika mashindano ya wazi, tumejiandaa vizuri na ninaamini tutarudi na medali za ushindi, " alisema Chunga.

Aliongeza amewataka wanariadha wake kufuata maelekezo waliyopata wakati wa mazoezi na endapo watatekeleza, watarejea nyumbani na matokeo mazuri.

"Mashindano haya yanayoshirikisha vijana kutoka nchi zote 11 za ukanda huu yatatusaidia kuwajenga wanariadha wetu chipukizi ambao watawakilisha nchi katika mashindano mengine yajayo," aliongeza kocha huyo.




Magolikipa wa Ihefu (Singida Black Stars), wakifanya mazoezi kwa ajili ya kujiandaa kuivaa Mashujaa FC katika mechi ya hatua ya robo fainali ya mashindano ya Kombe la FA itakayochezwa Mei Mosi, mwaka huu. **PICHA: MTANDAO**

# Kichuya apeleka sifa kwa Yanga

Na Adam Fungamwango

LICHA ya timu yake kulazimisha suluhu katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyochezwa juzi, winga wa JKT Tanzania, Shiza Kichuya, amesema Yanga ina kikosi bora zaidi msimu huu kuliko timu nyingine yoyote.

Akizungumza jijini, Dar es Salaam, Kichuya, winga wa zamani wa Simba, alisema kwa sababu amecheza mechi mbalimbali za Ligi Kuu na timu kadhaa, amegundua Yanga ina kikosi bora kwa sasa nchini.

"Ukiizungumzia Yanga, kwa sasa ni timu bora ukilinganisha na timu nyingine, nikisema hivyo nina maana iko bora kila sehemu, kila mchezaji wa timu hiyo ukipambana naye tu utagundua ana nguvu, lakini kila mmoja anaitendea haki namba anayocheza.

Lakini inaonekana kabisa wana ari ya kupambana, pia wanacheza kutokana na maelekezo ya walimu wao," alisema Kichuya.

Nyota huyo alisema timu yoyote inayotaka kucheza na Yanga ni lazima iingie na mpango mkakati na si kwenda kucheza tu, vinginevyo itakuwa na dakika 90 ngumu uwanjani.

"Sisi tulicheza kwa maelekezo ya walimu wetu baada ya kuwatazama Yanga, nguvu zao na udhaifu wao mdogo ambao tumeutumia. Kama uliona mwanzo tuliweka mabeki watatu, lakini kipindi cha pili walipomwingiza Bakari Mwamnyeto, sisi pia tuliweka mabeki watatu ili kuwaruhusu mawinga wao na mabeki wapande mbele kuongeza namba na kupiga krosi," alisema winga huyo.

Aliongeza timu yake haipo katika nafasi nzuri, lakini wanawahakikishia mashabiki wao watapambana kwa kila hali ili iondoke katika mstari wa hatari.

"Tunashukuru mashabiki walivyojitokeza kwa wingi kutushangilia, tunawaahidi hatutawaangusha, tutapambana ili kuibakisha timu Ligi Kuu na tumalize katika nafasi nzuri," Kichuya alisema.

Wakati huo huo, Kichuya, nyota wa zamani wa Mtibwa Sugar, amekanusha tetesi kwa sasa yeye ni askari baada ya kuhudhuria mafunzo ramsi ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT).

Alisema wengi walidhani hiyo kutokana na hivi karibuni kunyoa kipara, kitu ambacho alifanya kama 'fasheni' tu, lakini yeye bado ni raia.

JKT Tanzania kwa sasa imefikisha pointi 23, iko katika nafasi ya 13 kwenye msimamo wa ligi, ikiwa katika harakarati za kujiondoa katika mstari mwekundu wa kushuka daraja pamoja na kucheza mechi za mchujo.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### UNITED YAMTAKA TONEY

KLABU ya Manchester United inavutiwa na mshambuliaji wa Brentford na Timu ya Taifa ya England, Ivan Toney, 28, na wanaamini mchezaji huyo ataleta uzoefu na uongozi katika kikosi chao. ***(90min)***

### TONEY ANUKIA SPURS

TOTTENHAM Hotspur pia imeonyesha nia ya kujitosa kumwania mshambuliaji wa Brentford na England, Ivan Toney, kwa ajili ya kuimarisha safu yao ya mbele katika msimu ujao. ***(GivemeSport)***

### RASHFORD, CASEMIRO KUSEPA

KLABU ya Manchester United inalenga kuwaachia wachezaji 12 msimu huu wa joto, akiwemo fowadi wa Timu ya Taifa ya England, Marcus Rashford, 26, na kiungo wa kati wa Brazil, Casemiro (32). ***(Mirror)***

### POCHETTINO MAMBO MAGUMU

MUSTAKABALI wa Mauricio Pochettino kama kocha wa Chelsea upo katika mizani na unaweza kutegemea iwapo anaweza kufuzu kwa mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.***(Times)***

### OSIMHEN AKARIBIA PSG

MSHAMBULIAJI wa Napoli, Victor Osimhen, 25, anakaribia kujiunga na Paris Saint-Germain, lakini mshambuliaji huyo pia ameivutia Chelsea. ***(Il Mattino)***

### DIOMANDE KUTUA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United inaongoza katika kinyang'anyiro cha kumsajili beki wa kati wa Sporting Lisbon, Ousmane Diomande, 20, ambaye ana kipengele cha kutolewa cha euro milioni 80. ***(A Bola)***

### GALLAGHER ATAJWA SPURS

TOTTENHAM Hotspur ipo katika nafasi nzuri ya kumsajili kiungo wa kati wa England, Conor Gallagher, 24 kutoka Chelsea msimu huu - licha ya kumezewa mate na Newcastle. ***(Football Insider)***

### MENDY AGOMBEWA EPL

ARSENAL inataka kumnunua beki wa kushoto wa Real Madrid, Ferland Mendy, 28, huku Liverpool, Manchester United na Newcastle pia zikimtaka. ***(L'Equipe)***

### WILLIAMS KUTUA VILLA

KOCHA wa Aston Villa, Unai Emery anashinikiza klabu hiyo kumsajili winga wa Athletic Bilbao, Nico Williams, 21. ***(GiveMeSport)***

### SUMMERVILLE SOKONI

ASTON Villa inamfuatilia kwa karibu winga wa Leeds Utd, Crysencio Summerville, 22. ***(Football Insider)***

### SPURS KUIBEBA GENOA

TOTTENHAM Hotspur inaweza kuipa Genoa fursa ya kumsajili kwa mkopo beki wao, Djed Spence, 23, kwa mkataba wa kudumu kubadilishana na mshambuliaji wa Iceland, Albert Gudmundsson (26). ***(Calcio Mercato)***

## DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# KLOPP AKATA TAMAA KUBEBA TAJI LA EPL

**Kocha huyo sasa aziombea dua mbaya Arsenal na City...**

**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp amesema Liverpool inahitaji "makosa" ya Arsenal na Manchester City ili kufufua matumaini yao ya ubingwa wa Ligi Kuu England baada ya kipigo cha mabao 2-0 kwenye mechi ya dabi ya Merseyside dhidi ya Everton.

**Liverpool sasa wameachwa pointi tatu nyuma dhidi ya vinara Arsenal wenye pointi 77 zikiwa zimesalia mechi nne.**

Mabao ya Jarrad Branthwaite na Dominic Calvert-Lewin yaliipa Everton ushindi wa kwanza wa nyumbani wa dabi tangu mwaka 2010 na yote yalimaliza hofu ya kushuka daraja kwa kuwasogeza kwa pointi nane kutoka katika mstari wa hatari.

Mashabiki wa Everton waliwakejeli wapinzani wao kwa kuimba "Ulipoteza ligi kwenye Uwanja wa Goodison Park" na Klopp, ambaye atajiuzulu kama kocha wa Liverpool mwishoni mwa msimu huu, alisema timu yake sasa ina nafasi finyu katika mbio za ubingwa.

"Sijui kwa nini ninahitaji kujibu swali, lakini najua jinsi inavyofanya kazi," alisema Klopp.

"Unaweza kuona msimamo. Tunahitaji makosa ya Arsenal na City, kwa hiyo wao wanahitaji kushinda mechi kama ambavyo hatujafanya usiku wa leo (juzi). Arsenal na City lazima wawe na wakati mbaya sana ndio sisi tutakuwa na nafasi.

"Naomba radhi kwa siku ya leo (juzi) kwa mashabiki, tulipaswa kufanya vizuri zaidi lakini hatukufanya hivyo. Utendaji wetu haukuwa mzuri vya kutosha na nimesikitishwa sana.

"Tulishindwa kujilinda na tukawapa Everton mabao mawili na pengine wangeweza kuongeza."

Klopp aliongeza kuwa itabidi apate nafuu kimwili na kiakili, lakini sehemu ya pili ni ngumu unapopoteza mchezo kama huu.

"West Ham labda watakuwa wakitusubiri (Jumamosi) na kusugua mikono yao, wakitumaini kwamba wanaweza kufanya jambo, lakini lazima tupate nafuu kwa hilo," alisema Klopp.

Ushindi wa Everton ulipokelewa kwa shangwe na mashabiki wa nyumbani, ambao walibaki Goodison Park kuimba na kuwapongeza wachezaji wao muda mrefu baada ya filimbi ya mwisho.

Naye Kocha wa Everton, Sean Dyche, alisema ushindi huo ni wa mashabiki ambao wamevumilia msimu wa hali mbaya kufuatia kupunguzwa kwa pointi.

"Ushindi huo ni wa watu," alisema Dyche.

# XAVI AKUBALI KUBAKIA BARCA



**BARCELONA,** Hispania

XAVI Hernandez amekubali kubakia kama kocha wa Barcelona hadi mwisho wa mkataba wake mwaka 2025 na kubatilisha uamuzi wake wa kujiuzulu, kwa mujibu wa ESPN.

Xavi mwenye umri wa miaka 44 alitangaza Januari, mwaka huu ataondoka kwenye wadhifa huo mwishoni mwa msimu kufuatia msururu wa matokeo mabaya, akisema kazi hiyo pia imemsumbua kikili.

Hata hivyo, baada ya mkutano na Rais, Joan Laporta, hapo juzi, mchezaji huyo wa zamani wa kimataifa wa Hispania ameamua kutimiza ahadi yake ya kimkataba na klabu hiyo ya Katalunya.

Makamu wa Rais wa Barcelona, Rafa Yuste, alionekana kuthibitisha makubaliano hayo alipotoka katika mkutano huo Jumatano usiku.

"Tulikuwa na mkutano na kocha na rais ambapo Xavi alituonyesha kujitolea kwake," aliwaambia waandishi wa habari.


"Yeye ni kijana wa Barca, ndiye kocha anayeweza kuongoza mradi wetu na wachezaji wetu wachanga. Nina hakika atafanya kazi kubwa, nina furaha sana kwake.

"Nina furaha na Xavi kubaki kwa sababu siku zote nilitetea mwendelezo wa mradi alioanzisha miaka miwili na nusu iliyopita.

"Hatujazungumza katika mkutano kuhusu mabadiliko katika timu yetu hata kidogo. Xavi ameonyesha shauku yake na lazima tumuunge mkono yeye na wafanyakazi wake kuendelea na mradi huu."

Xavi aliteuliwa kuwa Kocha wa Barca mwaka, 2021, na kuwaongoza kutwaa taji lao la kwanza la ligi katika miaka minne msimu uliopita na kutia saini nyongeza ya mkataba hadi Juni 30, 2025, kukiwa na chaguo la mwaka mmoja zaidi.

# Afya ya Carlos Tevez yaimarika



**BUENOS AIRES,** Argentina

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Manchester United na Manchester City, Carlos Tevez yuko katika hali "ya kuridhisha" baada ya kukimbizwa hospitalini akiwa na maumivu ya kifua.

Tevez alipelekwa katika kliniki ya Kitongoji cha San Isidro huko Buenos Aires Jumanne, ambako alikaa usiku huo kabla ya kufanyiwa vipimo zaidi vya afya.

Tevez mwenye umri wa miaka 40 kwa sasa ni Kocha Mkuu wa Independiente ya Argentina - nafasi ambayo alichukua Agosti, mwaka jana kwa mkataba wa muda mfupi kabla ya kuongezewa utakaoendelea hadi Desemba mwaka, 2026.

Taarifa ya klabu hiyo kuhusu hali ya Tevez ilisema: "Kocha wetu Carlos Tevez alikwenda katika hospitali ya La Trinidad iliyopo San Isidro akiwa na maumivu ya kifua, walifanya vipimo vilivyolingana na vimeridhisha, leo (jana) ataendelea na mfululizo wa vipimo."

Independiente baadaye walifafanua Tevez angebakia hospitalini kama 'tahadhari' huku madaktari wakikusudia kufanya vipimo zaidi.

Tevez alifurahia wakati wa uchezaji wake wa kiwango cha juu, akiwakilisha Argentina michezo 76 katika kipindi cha miaka 11.

Baada ya kujulikana katika klabu ya Corinthians, alijiunga na West Ham United Agosti mwaka, 2006 pamoja na raia mwenzake Javier Mascherano, lakini makubaliano hayo yalibainika yamekiuka kanuni za Ligi Kuu England.

Uhamisho wa kwenda Inter ulishindikana kabla ya Tevez kujiunga na Manchester United msimu wa joto wa mwaka 2007, kwa mkataba mgumu wa mkopo wa miaka miwili.

# Manchester Utd yamtolea macho Toney

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United inavutiwa na mchezaji wa Brentford, Ivan Toney, katika kutafuta mshambuliaji mpya msimu huu wa joto, kwa mujibu wa 90min.

Toney yuko tayari kuachana na Nyuki hao msimu huu wa joto au ifikapo mwakani wakati mkataba wake wa sasa utakapomalizika.

Brentford wanatarajiwa kutaka ada ya angalau pauni milioni 50, ingawa hii inaweza kubadilika kulingana na ushiriki wake na uchezaji wake katika michuano ya Euro 2024 akiwa na England.

Vyanzo vimeiambia 90min, United wanamtaka Toney na wanaamini ataleta uzoefu na uongozi katika chumba chao cha kubadilishia nguo.

United wamefanya usajili wa mshambuliaji mpya wa kati kusaidia na kushindana na Rasmus Hojlund, kuwa kipaumbele katika dirisha la usajili la majira ya joto.

Wakati mchezaji wa RB Leipzig, Benjamin Sesko - ambaye mkataba wake una kipengele cha kuachiliwa kwa pauni milioni 43 - kwa sasa yuko juu kwenye orodha ya wachezaji wanaowaniwa na United kuliko Toney, inakubalika watakabiliwa na ushindani mkubwa zaidi kwa nyota huyo wa Slovenia.

Hivyo mshambuliaji huyo wa Brentford bado anaweza kuwa chaguo ikiwa ada ya Brentford itapungua.



HABARI MICHEZO

# NAMUNGO YATAMBA KUIPA KICHAPO SIMBA JUMATATU

Na Shufaa Lyimo

BENCHI la ufundi la Namungo FC limesema linaendelea kuimarisha safu yake ya ushambuliaji kwa ajili ya kuhakikisha haipotezi mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Simba utakaochezwa Aprili 29, mwaka huu kwenye Uwanja wa Majaliwa mkoani, Lindi.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa Namungo, Mwinyi Zahera, alisema lengo la kuboresha idara ya ushambuliaji ni kuhakikisha wachezaji wake wanatumia vyema nafasi wanazopata na hatimaye kuzibakisha pointi tatu nyumbani.

Zahera alisema wataingia katika mechi hiyo kwa tahadhari kwa sababu wanaamini Simba pia itahitaji kupata ushindi na kuendelea kujiimarisha katika msimamo wa ligi hiyo.

**"Kwa sasa nashughulika na safu ya ushambuliaji ili nipate matokeo mazuri katika mchezo dhidi ya Simba, mchezo huo unatarajiwa kuwa na upinzani mkubwa," alisema Zahera.**

Kocha huyo aliongeza kwake kila mchezo ni muhimu kwa sababu anahitaji kumaliza msimu katika nafasi za juu lakini pia kuwapa furaha mashabiki wao.

"Tunaupa umuhimu mkubwa mchezo huo kwa sababu tunafahamu tunakutana na timu ambayo imetoka kushiriki mashindano ya kimataifa, vile vile ina wachezaji wengi wa kimataifa wenye uzoefu," Zahera alisema.

Aliongeza mchezo huo utakuwa ni mwendelezo wa maandalizi ya mechi ya hatua ya robo fainali ya mashindano ya Kombe la FA dhidi ya Azam FC utakaopigwa ifikapo Mei 3, mwaka huu kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Alisema pia wachezaji wote wanaendelea vyema isipokuwa mchezaji wake mmoja Fabrice Ngoma ambaye amevunjika mguu.

"Fabrice amevunjika mguu kwa mujibu wa Daktari wetu hawezi kuonekana uwanjani mpaka msimu ujao kutokana na hali yake ilivyo, " aliongeza Zahera.

Naye Katibu Mkuu wa timu hiyo, Ally Mkadeba, alisema mikakati yao ni kupata pointi tatu na uwezo wa kufanya hivyo wanao.

"Tuna matumaini makubwa ya kumfunga Simba, tuko kamili kila idara kuwakabili, tumejipanga vyema kuhakikisha tunafikia malengo," alisema Mkadeba.

# Bilioni 19 zatengwa kuukarabati

INATOKA UKURASA 24

wa Azam Complex nao utafungwa kwa muda ili kufanyiwa maboresho.

"Sawa tumempa miezi 12, lakini tumemwomba ndani ya miezi sita uwe umakamilika kwa sababu ya uchache wa viwanja hapa Tanzania, tumezungumza na mkandarasi tunahitaji uwanja ukamilka mapema, Azam Complex ukija kufungwa itakuwa tabu kwa ligi kuchezwa, hivyo tunauhitaji Uwanja wa Uhuru mapema," alisema Msigwa.

Aliongeza uwanja huo ukitumika ipasavyo utasaidia kupunguza matumizi ya Uwanja wa Benjamin Mkapa, lakini pia utatoa fursa kwa Tanzania mwenyeji wa kuandaa mashindano mbalimbali ya kimataifa.

"Tunauhakika na wakandarasi tuliowapa, kwa sababu tunawafahamu na tunaimani watafanya kitu kizuri, Uwanja wa Uhuru unaingiza watu 23,000, lakini tunahitaji kupandisha hadi 30,000.

Tutajadiliana na mkandarasi wa Uwanja wa Uhuru kuondoa sehemu ya kukimbilia riadha na kuongeza vitu ili kupanda daraja (kutoka daraja la tatu hadi daraja la pili) katika viwango vya Shirikisho la Soka la Kimataifa (FIFA)," alisema Msigwa.

Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wallace Karia, alisema tukio la kusaini mkataba huo ni jambo kubwa kwa sababu Uwanja wa Uhuru, una historia na anaahidi kushirikana na serikali katika kupata viwanja vizuri kwa ajili ya kutumika katika mazoezi.

"Ukarabati wa Uhuru utakuwa na faida kubwa sana kwetu, kwa sababu baada ya AFCON, utatumika kwa ajili ya timu kucheza michezo ya mbalimbali ikiwamo Ligi Kuu Tanzania Bara," alisema Karia.

Ukarabati wa uwanja huo ni mwendelezo wa ujenzi wa viwanja kama sehemu ya maandalizi ya mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2027), ambayo Tanzania, Kenya na Uganda watakuwa wenyeji.




Katibu Mkuu wa Wizara ya Utamaduni Sanaa na Michezo, Gerson Msigwa (kulia) akisaini mkataba wa makubaliano ya ukarabati wa Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam. Kushoto ni mwakilishi kutoka katika Kampuni ya Ujenzi kutoka China (CRCEG) kwa ajili ya ukarabati wa Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam. **PICHA: SAADA AKIDA**

# Maregesi awaza tiketi Olimpiki

Na Shufaa Lyimo

BONDIA wa ngumi za ridhaa nchini, Mussa Maregesi, amesema anajiimarisha kwa ajili ya kwenda kufanya vizuri katika mashindano ya kusaka tiketi ya kushiriki Michezo ya Olimpiki itakayofanyika kati ya Mei 20 na Juni 2, mwaka huu nchini Thailand.

Akizungumza na Nipashe jana, Maregesi alisema anajipanga vyema kuhakikisha anafikia malengo yake kwa kufanya vizuri katika mashindano hayo ambayo anatarajia kukutana na ushindani.

Maregesi alisema bado anaamini ndoto zake za kushiriki Michezo ya Olimpiki itakayofanyika baadaye mwaka huu itatimia.

"Malengo yangu ni kwenda kufanya vizuri katika mashindano haya, nitaamini nitarudi nyumbani na medali ya dhahabu, ninaenda kupeperusha vyema bendera ya Tanzania," alisema Maregesi.

Aliongeza anatarajia kuingia kambini rasmi wiki ijayo ili kuendelea na maandalizi na anawashukuru wote wanaompa ushirikiano katika kuboresha kiwango chake.

"Ninaendelea kujipanga ili kuhakikisha ninaenda katika mashindano hayo nikiwa vizuri, ninawaomba Watanzania waendelee kuniunga mkono," Maregesi alisema.

Bondia huyo pia amemshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa zawadi ya fedha alizompa baada ya kufanya vizuri katika Michezo ya All African Games yaliyofanyika Ghana Machi, mwaka huu ambapo alipata medali tatu za shaba.

# Gamondi alalamikia uwanja, JKT kicheko

INATOKA UKURASA 24

tumetoa sare kutokana na hali mbaya ya uwanja," alilalamika kocha huyo.

Hata hivyo, baadaye Gamondi alisema wapinzani wao walitengeneza nafasi mbalimbali katika kipindi cha kwanza ambazo hawakuzitumia vyema, lakini kipindi cha pili wachezaji wake wakalazimika kuzoea changamoto ya uwanja.

"Na mimi pia nashukuru kwa kupata pointi moja kwa sababu tumecheza katika mazingira magumu ya uwanja na hali ya hewa pia," kocha huyo wa zamani wa Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini, alisema.

Naye Kocha Msaidizi wa JKT Tanzania, George Mketo, alisema waliwasoma vyema Yanga katika michezo yao mitatu iliyopita na kuandaa mpango mkakati, ikiwamo kumfanya kiungo mshambuliaji, Stephane Azi Ki, asiwe huru na mpira kutokana na kupenda kupiga mashuti ya mbali.

"Tuliwasoma Yanga zaidi ya michezo mitatu nyuma, tulijua ina wachezaji wenye nguvu, na wanategemea sana kupitisha pembeni mashambulizi yao, na mtu mwingine ambaye ni hatari tuliyemwekea mikakati ni Aziz Ki, anashuka chini kuchukua mpira ili kutengeneza nafasi za kupiga mashuti, tukaweka mabeki watatu kati ili yeye na wenzake wasiweze kupata nafasi ya kupiga, na hilo tumefanikiwa," alisema Mketo.

Kocha huyo aliwapongeza wachezaji wake akisema walicheza ndani ya mpango waliupanga katika kikao uwanja wa mazoezi yaliyochukua wiki mbili.


Matokeo ya mchezo huo yameifanya Yanga imeendelea kujiimarisha kileleni ikifikisha pointi 59, ikihitaji pointi 15 ili kutetea taji la ubingwa wanaloloshikilia.

Endapo Simba itashinda mechi zake tisa zilizosalia itafikisha pointi 73 huku Azam iliyoko nafasi ya pili kwenye msimamo, imebakisha michezo sita, ikifanikiwa kushinda, itafikisha pointi 72.

# Michezo

Ijumaa Aprili 26, 2024

Nipashe

## Afya ya Tevez yaimarika

UKURASA 22



Mshambuliaji wa Simba Queens, Aisha Mnunka (aliyeruka juu), akipambana kuwania mpira dhidi ya wachezaji wa Yanga Princess katika mechi ya Ligi Kuu ya Soka ya Wanawake Tanzania iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam jana. Simba Queens ilishinda mabao 3-1. **PICHA: MTANDAO**

## Bilioni 19 zatengwa kuukarabati Uhuru



**Na Saada Akida**

WIZARA ya Utamaduni, Sanaa na Michezo imesaini mkataba na Kampuni ya Railway Construction Engineering Group (CRCEG) kutoka China wenye thamani ya Sh. bilioni 19.7 kwa ajili ya ukarabati wa ujenzi wa Uwanja wa Uhuru ulioko, Dar es Salaam.

Ukarabati wa uwanja huo maarufu Shamba la Bibi unatarajiwa kuchukua mwaka mmoja na utafanyika katika vyumba vya kubadilishia nguo, kuta za uwanja, ubao wa kuonyesha matokeo, mifumo ya sauti, sehemu ya kukimbia riadha, kuweka kamera za usalama na eneo la kuchezea (pitch).

Akizungumza katika hafla ya kusaini mkataba huo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Gerson Msigwa, alisema licha ya kumpa muda wa mwaka mmoja mkandarasi huyo, lakini wamemwomba ikiwezekana kukamilisha ukarabati huo ndani ya miezi sita.

Msigwa alisema anaamini ukarabati huo unaweza kukamilika mapema kwa sababu ya uhaba wa viwanja haoa nchini hasa Dar es Salaam ambayo itapata upungufu kutokana na Uwanja

INAENDELEA UKURASA 23

# GAMONDI ALALAMIKIA UWANJA, JKT KICHEKO

**Na Adam Fungamwango**

### ●●● Maafande hao watamba 'waliikamata roho' ya Yanga katika...

BAADA ya kulazimishwa suluhu na JKT Tanzania katika mechi ya Ligi Kuu Bara, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema sababu iliyowanyima ushindi katika mchezo huo ni hali mbaya ya Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo iliyotokana na mvua zinazoendelea kunyesha Dar es Salaam.

Mechi hiyo ilichezwa kwenye uwanja uliojaa maji na matope hasa katika eneo la katikati na kusababisha mpira kushindwa kudunda, awali mchezo huo ulipangwa kufanyika Jumanne.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Gamondi ambaye timu yake ilipunguzwa kasi katika mbio za ubingwa alisema hali ya uwanja haikuwa rafiki na haukupaswa kutumika kwa mechi hiyo ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

**Gamondi alisema timu yake haiwezi kucheza vyema katika uwanja wa aina ile na hawezi kutoa tathmini ya mechi namna ilivyokuwa.**

"Huwezi kucheza vyema kwenye uwanja wa aina hii, huwezi kucheza mpira wa mfumo na kiufundi namna hii, nataka kujua kwa nini tulihitajika katika uwanja huu?" alihoji Gamondi.



Kocha huyo, ambaye ni raia wa Argentina, alisema alivyoona wachezaji wa JKT Tanzania walikuwa wazuri zaidi kucheza kwenye matope kuliko wachezaji wake ambao ndio vinara wa ligi hiyo.

"Siwezi kuzungumza tumechezaje na madhaifu yaliyoonekana wakati wachezaji wangu walikuwa ndani ya uwanja wenye hali kama hii, wao JKT Tanzania nimeona ni wazuri kucheza katika hali hii, nadhani ndiyo maana wametulazimisha kucheza hapa. Siwezi kutoa tathmini, si unaona wanafuraha sana, naona watu wengi wamefurahi kwa sababu

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >